# MATUMIZI YA MAJADILIANO YA VIKUNDI KATIKAKUFUNZIA STADI YA KUZUNGUMZA KATIKA SHULE ZA UPILI KATIKATARAFA YA MOSOCHO, KAUNTI YA KISII, KENYA.


MAGARE DANIEL YUVINALIS

E55/CE/23556/2011


TASNIFU HII YA UTAFITI IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI

YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

**JUNE, 2017**

**UNGAMO**

Tasnifu hii **y**a utafiti ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

Sahihi…………………………………………………..Tarehe……………

Magare Daniel Yuvinalis

E55/EC/23556/2011

Tasnifu hii ya utafiti imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi…………………………………………..Tarehe……………………

Dkt. Hamisi Omar Babusa

Idara ya mawasiliano na Teknolojia ya elimu,chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi…………………………………………………Tarehe…………………

Prof. Samson Ondigi

Idara ya mawasiliano na Teknolojia ya elimu,chuo kikuu chaKenyatta.

## KUTABARUKU

Ninatabaruku kwa Mola kwa kunipa siha njema katika kipindi chote cha kufanya utafiti huu.Wazazi wangu, mke wangu Bonareri na watoto wangu Brenda, Stacy, Whitney na Magare Jnr pia sitawasahau kwa kunipa moyo na kuniandalia mazingira bora ya kusomea shahada hii ya uzamili.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt Hamisi Omar Babusa na Prof. Samson Ondigi kwa kunipa mwongozo mzuri katika kufanya utafiti huu kuanzia uchaguzi wa mada, uandishi wa pendekezo na tasnifu . Shukrani pia ziwaendee wahadhiri wote walionifunza masomo yote katika digrii yangu ya uzamili. Shukrani nyingine pia ziwafikie walimu na wanafunzi walioshiriki katika hatua zote za ukusanyaji data. Mola awabariki nyote kwa msaada wenu katika kufanikisha kazi hii.

# YALIYOMO

**UNGAMO** .......... **ii**
**KUTABARUKU** .......... **iii**
**SHUKRANI** .......... **iv**
**YALIYOMO** .......... **v**
**ORODHA YA MICHORO** .......... **ix**
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **x**
**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... **xi**
**ABSTRACT** .......... **xii**
**IKISIRI** .......... **xiii**
**SURA YA KWANZA** .......... **1**
**1.1 Utangulizi** .......... **1**
**1.2 Usuli Wa Utafiti** .......... **1**
**1.4 Lengo la Utafiti** .......... **5**
**1.5 Madhumuni ya Utafiti** .......... **5**
**1.6 Maswali ya Utafiti** .......... **6**
**1.7 Umuhimu wa Utafiti** .......... **6**
**1.8 Machukulio ya Utafiti** .......... **7**
**1.9 Mipaka ya Utafiti** .......... **7**
**1.10 Msingi wa Kinadharia** .......... **7**
**1.11 Mhimili wa Dhana ya Utafiti** .......... **9**
**1.12 Ufafanuzi wa Istilahi** .......... **11**
**SURA YA PILI** .......... **13**
**YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA** .......... **13**
**2.1 Utangulizi** .......... **13**
**2.2 Dhana ya majadiliano ya vikundi na uundaji wa vikundi** .......... **13**
**2.3 Shughuli zifanywazo vikundini zihusianazo na stadi ya kuzungumza** .......... **15**

**2.4 Majukumu ya mwalimu na mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi. . 16**

2.4.1 Majukumu ya mwalimu katika majadiliano ya vikundi ........................... 16

2.4.2 Majukumu ya mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi ........................ 17

**2.5 Manufaa ya Majadiliano ya Vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza ....... 18**

**2.6 Changamoto Zikabilizo Majadiliano Katika Vikundi ................................ 20**

**2.7 Muhtasari wa yaliyoandikwa kuhusu mada na pengo la utafiti................. 20**

**SURA YA TATU ........................................................................................... 22**

**MBINU ZA UTAFITI. .................................................................................. 22**

**3.1 Utangulizi.................................................................................................. 22**

**3.2 Muundo wa Utafiti ................................................................................... 22**

**3.3 Mahali pa Kufanyia Utafiti...................................................................... 23**

**3.5 Sampuli na Mchakato wa Uteuzi wa Sampuli.......................................... 23**

**3.6. Vifaa Vya Kukusanya Data ..................................................................... 24**

**3.7. Majaribio Ya Vifaa Vya Utafiti ................................................................ 25**

3.7.1 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti ..................................................................... 25

3.7.2 Utumainifu wa Vifaa vya Utafiti ............................................................. 26

**3.8 Utaratibu Wa Kukusanya Data .................................................................. 26**

**3.9 Uchanganuzi wa Data................................................................................ 27**

**3.10 Swala la maadili........................................................................................ 28**

**SURA YA NNE.............................................................................................. 29**

**UWASILISHAJI WA DATA,UCHAMBUZI NA MAELEZO ........................... 29**

**4.1 Utangulizi.................................................................................................. 29**

**4.2 Wasailiwa walengwa ................................................................................. 29**

**4.3 Maelezo ya wanafunzi kuhusu majadiliano katika vikundi shuleni........... 33**

**4.4 Shughuli zihusishwazo katika kufundishia stadi ya kuzugumza vikundini katika muktadha wa majadiliano ya vikundi ................................................. 35**

**4.5 Majukumu katika majadiliano katika Vikundi** ........................................ **38**

**4.6 Manufaa wa Majadiliano ya Vikundi** ........................................................ **40**

4.6.1 Maelezo ya Wanafunzi kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi ......... 40

4.6.2 Maelezo ya walimu kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi ............. 42

4.6.3 Uchanganuzi wa matokeo ya mtihani wa kwanza na wa mwisho ............. 44

**4.7 Changamoto zikumbazo Majadiliano ya Vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza** ........................................................................ **48**

**SURA YA TANO** ................................................................................ **52**

**HITIMISHO YA MADHUMUNI YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO** ........... **52**

**5.1 Utangulizi** ....................................................................................... **52**

**5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti** .............................................................. **52**

**5.3 Hitimisho** ........................................................................................ **54**

**5.4 Mapendekezo** ................................................................................... **55**

**5.5 Mapendekezo ya Utafiti wa baadaye** ..................................................... **57**

**MAREJELEO** ......................................................................................... **58**

**VIAMBATISHO** ..................................................................................... **61**

**KIAMBATISHO I: HOJAJI KWA WANAFUNZI** ........................................ **61**

**KIAMBATISHO II: HOJAJI KWA WALIMU** ............................................. **63**

**KIAMBATISHO III: MTIHANI KWA WANAFUNZI TEULIWA** ............... **64**

**KIAMBATISHO IV: ALAMA WASTANI ZA MTIHANI WA KWANZA KATIKA SHULE SITA TEULIWA.** ................................................................ **65**

**KIAMBATISHO V: ALAMA WASTANI ZA MTIHANI WA MWISHO KATIKA SHULE SITA TEULIWA** ................................................................ **66**

**KIAMBATISHO VI: BARUA YA KIBALI KUTOKA CHUONI** .................. **67**

**KIAMBATISHO VII: BARUA YA UTAMBULISHO** .................................... **68**

**KIAMBATISHO VIII: RAMANI YA KISII YA KATI** .................................. **69**

**KIAMBATISHO IX: SHULE ZA SEKONDARI KISII YA KATI ................ 70**

**KIAMBATISHO X: LESENI YA UTAFITI KUTOKA NACOSTI................ 71**

**KIAMBATISHO XI: KIBALI KUTOKA NACOSTI ...................................... 72**

# ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Mhimili wa Dhana Ya Utafiti ................................................................. 10

Mchoro 2: Mawasiliano katika vikundi ................................................................... 15

Mchoro 3: Chati inayoonyesha maelezo ya walimu kuhusu majadiliano vikundini... 35

Mchoro 4: Chati inayoonyesha wajibu wa waalimu katika majadiliano vikundini ... 39

Mchoro 5: Chati inayoonyesha maelezo ya wanafunzi kuhusu manufaa ya Majadiliano ya Vikundi ........................................................................................... 41

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1 Uteuzi wa sampuli. ..................................................................... 24

Jedwali 4.1 Idadi ya wasailisiwa wanafunzi na walimu. ......................................... 29

Jedwali 4.2 Wanafunzi wasailiwa ........................................................................... 30

Jedwali 4.3 Jinsia wanafunzi na walimu ................................................................ 31

Jedwali 4.4: Kidato cha mwanafunzi ...................................................................... 31

Jedwali 4.5 Kiwango cha masomo cha walimu ...................................................... 32

Jedwali 4.6 Maelezo ya wanafunzi na walimu kuhusu aina ya shule ........................ 32

Jedwali 4.7 Maelezo ya wanafunzi kuhusu majadiliano ya vikundi. ......................... 34

Jedwali 4.8: Maelezo ya wanafunzi kuhusu shughuli zifanywazo katika majadiliano vikundini ............................................................................................................... 36

Jedwali 4.9: Maelezo ya walimu kuhusu Shughuli zifanywazo katika majadiliano vikundini ............................................................................................................... 37

Jedwali 4.10 Maelezo ya wanafunzi kuhusu wajibu wao katika majadiliano vikundini. ............................................................................................................... 38

Jedwali 4.11: Maelezo ya walimu kuhusu manufaa ya majadiliano katika vikundi. .. 43

Jedwali 4.12: Matokeo linganishi ya mtihani wa kwanza na mwisho kuchunguza manufaa ya majadiliano ya vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza. ......................... 45

Jedwali 4.13: Maelezo ya wanafunzi kuhusu changamoto katika majadiliano vikundini ............................................................................................................... 49

Jedwali 4.14: Maelezo ya walimu kuhusu changamoto za majadiliano vikundini. .... 50

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| NACOSTI | National Commission for Science and Technology and Innovation |
| SPSS | Statistical Package for Social Science |
| QASO | Quality Assurance and Standards Officer |

## ABSTRACT

This study investigated the use of group discussion method in teaching speaking skill among secondary school students in Mosocho division, Kisii County, Kenya.The problem investigated in the study was that most students in secondary school are not able to communicate fluently in Kiswahili.The purpose of the study was to investigate the effectiveness of group discussion method in teaching speaking skill.The objectives of the study were to find out whether group discussions may enhance speaking skill and to investgate the role of the teacher and students in group discussions in classroom stuation.The assumption of the study was that respondents would give the correct information about use of group discussion method and that the sample represented the target population.The study is significant to teachers, students, education officials and other researchers. The study was guided by role theory by Robert Owen of 1998. Literature related to the study from other writers was reviewed. The research used Quasi-experimental design because two groups were involved.The locale of the study was Mosocho division in Kisii county and target population was secondary school students and teachers teaching Kiswahili. Asample of six schools were selected from fifteen schools through stratified sampling representing 40% of the population.The sample involved four hundred and eighty students 20% of the target population, twelve teachers representing 40% of the target population and six principals from the selected schools selected through purposive sampling.The instruments of data collection included; questionares sent to teachers and students and pretest and post-test for students in the selected schools. Piloting was done in two schools which were not included in the proper research to test the reliability of research instruments after which a test retest method was used to ascertain coeficient of reliability of r= 0.73 strong enough for the research instruments. Content validity was ascertained by consulting my supervisors.The questionares were administered to teachers and students and data collected was analysed using SPSS. The students were given two tests ( pre-test & post-test) whose result was analyzed using measures of central tendencies eg mean & range and spearmans correlation coefficient. The result was presented by graphs, piecharts and tables.The result of the study showed that group discussions enhance speaking skills among the students invoved.This study will benefit teachers, students and Quality Assurance & Standards officer(QASO). Indeed there is astrong relationship between use of group discussion method and speaking skill among stundents involved. Ethical issues were upheld by not including the names of respondents in the instruments of the study and making correct references to others writers work.The study recommends that teachers use group discussion method for teaching speaking skill in order to improve students' speaking skills.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ufaafu wa matumizi ya mbinu majadiliano ya vikundi katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, nchini Kenya. Swala la utafiti ni kuwa wanafunzi wengi wa shule za upili hukosa umilisi wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza ufaavu wa mbinu ya majadidiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza. Madhumuni ya utafiti huu ni kuchunguza ufaafu wa mbinu majadiliano ya vikundi katika ufundishaji wa stadi ya kuzungumza, aidha kutambua majukumu ya mwalimu na wanafunzi katika majadiliano ya vikundi. Machukulio ya utafiti ni kuwa wasailiwa watatoa majibu sahihi kuhusu matumizi ya majadiliano ya vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya majukumu ya Robert Owen ya mwaka1998 . Maandishi ya waandishi wengine yalichunguzwa ili kuchunguza ufaafu wa mbinu ya majadiliano ya vikundi katika kufundishia stadi ya kuzungumza. Muundo wa utafiti uliotumiwa katika utafiti huu ni wa majaribio kwa vile makundi mawili yalihusishwa. Mahali pa kufanyia utafiti ni tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii na wasailiwa walengwa walikuwa wanafunzi wa shule za upili na walimu wafundishao Kiswahili katika shule zilizoteuliwa. Sampuli ya shule sita kutoka shule kumi na tano ziliteuliwa kupitia sampuli tabakishi hii ikiwakilisha 40% ya shule lengwa. Sampuli ilihusisha wanafunzi 480 ikiwakilisha 20% ya walengwa, walimu 12 wafunzao Kiswahili ikiwakilisha 40% ya walengwa na walimu wakuu sita katika shule husika waliteuliwa kupitia sampuli maksudi. Ukusanyaji data ulifanywa kupitia hojaji kwa walimu na wanafunzi na mtihani wa mwanzoni na wa mwisho kwa wanafunzi katika shule zilizoteuliwa. Vifaa vya ukusanyaji data vilifanyiwa majaribio ili kuhakikisha uhalali na utumainifu wao kwa kutumia shule mbili ambazo hazikuhusishwa katika utafiti kamili. Baada ya majaribio yaliyorudiwa, uwiano ulionyesha kiwango cha r=o.73 cha kutegemewa katika utumainifu.Uhalali ulithibitishwa na wasimamizi wangu. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya SPSS na vipimo vya ukatikati kwa mtihani wa kwanza na mwisho pia kipimo cha uwiano cha spearman kubainisha uhusiano. Matokeo yaliwasilishwa kwa chati, grafu na majedwali. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha majadiliano ya vikundi yanaimarisha stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi wahusishwa. Utafiti huu ni muhimu kwa walimu wanaofundisha lugha na maafisa wa kukadria ubora wa elimu (QASOS). Kwa hakika kuna uwiano mkubwa baina majadiliano ya vikundi na umilisi wa stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi waliohusishwa kuliko wale ambao hawakuhusishwa. Maadili ya utafiti yalizingatiwa kwa kutohusisha majina ya walengwa katika vifaa vya utafiti na kufanya unukuzi sahihi wa maandishi ya wengine.Utafiti huu unapendekeza walimu watumie majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzingumza darasani ili kuimarisha umilisi wa stadi ya kuzungumza.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza ufaafu wa matumizi ya mbinu majadiliano ya vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.

Sura hii iliangazia mambo kama vile; usuli wa utafiti, suala la utafiti, lengo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, machukulio ya utafiti, mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia, mhimili wa dhana na ufafanuzi wa istilahi zilizohusiana na mada iliyotafitiwa.

## 1.2 Usuli Wa Utafiti

Mbinu za ufundishaji ni kigezo muhimu katika ufundishaji na kuboresha stadi za lugha ya Kiswahili ambazo ni; kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika. Kwa vile lengo kuu la lugha ni kuwasiliana, stadi ya kuzungumza yafaa kuangaziwa zaidi katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Stadi hii huhitaji matumizi ya mbinu zinazoweza kushirikisha wanafunzi katika kutoa maoni yao darasani ili kukuza uwezo wao wa kuwasliana kwa ukakamavu na ufasaha. Mbinu zinazotumiwa kufundishia lugha hutegemea vigezo kama; mada inayofunzwa, umri wa wanafunzi, kiwango cha uelewaji, madhumuni na stadi inayohusika.

Ujuzi wa mwalimu, tajriba yake na mbinu za kuelekeza wanafunzi darasani ni muhimu wakati wa kuchagua mbinu za kufundishia. Kuna mbinu za ufundishaji za kale ambazo zinaegemea mwalimu. Katika mbinu hizi mwalimu ndiye anaongoza

shughuli za masomo. Mfano wa mbinu hizi ni mihadhara na mijadala darasani, kazi mradi na majadiliano ya vikundi.

Kulingana na Kimemia (2001) mbinu za kale zimepitwa na wakati na hazisaidii wanafunzi kukuza stadi ya kuzungumza kwa ufasaha. Mbinu za kisasa zinaegemea mwanafunzi zaidi. Mifano ya mbinu hizi ni majadiliano ya vikundi, kazi mradi na ziara nyanjani. Katika mbinu hizi majadiliano ya vikundi hupendwa zaidi katika taasisi za masomo ya juu kwa vile ni rahisi kutumia na yanaweza kutumiwa pamoja na mbinu zingine za ufundishaji. Utafiti huu ulilenga kuchunguza ufaafu wa mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika shule za upili.

Kulingana na Galanes na Adams (2013) majadiliano ya vikundi huimarisha stadi ya mawasiliano na kuwapa wanafunzi nafasi kutoa maoni yao. Shughuli za darasani zinafaa kuhusisha wanafunzi zaidi katika kupokezana maoni wanaposhughulikia mada fulani. Wanafunzi ambao huogopa kuongea katika darasa hulazimika kutoa maoni ya katika vikundi hivyo kukuza stadi ya mawasiliano.

Kulingana na Gathumbi na Masembe (2005) kusikiliza na kuzungumza ni viungo muhimu katika ufundishaji wa lugha kwa vile zote hutokea katika mazingira sawa.Wanafunzi wengi wana matatizo katika kuhusisha stadi hizi mbili kwa hivyo huhitaji kuangaziwa zaidi katika ufundishaji. Wanafunzi hukosa ufasaha wa lugha kwa vile wanakosa kushirikishwa katika stadi ya kusikiliza na kuongea. Stadi hizi mbili zinafaa kuhusishwa wakati wa kufundisha stadi zingine za lugha.

Kulingana na Kimemia (2001) mbinu wanazotumia walimu kufundishia lugha ya Kiswahili zimepitwa na wakati. Walimu wengi hutumia mbinu ya kuongea na kutumia chaki ambapo wanafunzi hubugia tu wafunzwayo bila kupewa nafasi kutoa maoni. Alipendekeza mbinu za kufundisha zichunguzwe ili kumwezesha mwanafunzi kuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili hasa kuzungumza kwa ufasaha. Baadhi ya maeneo yaliyo na matatizo katika ufundishaji wa Kiswahili ni Kisii na Machakos.Tarafa ya Mosocho ni sehemu ya Kaunti ya Kisii. Tarafa hii pia imepakana na jiji la Kisii na shule nyingi zimo viungani mwa jiji la Kisii na wanafunzi wengi wa shule za mjini wameathiriwa na sheng.

Kulingana na Babusa (2010) walimu wanaofundisha Kiswahili wanafaa kuboresha ufundishaji wao kwa kutilia mkazo stadi zote za lugha. Walimu wengi hufundisha tu stadi andishi na kupuuza stadi zingumzi kwa vile wanafunzi hutahiniwa katika stadi andishi katika mitihani. Walimu hufundisha wanafunzi jinsi ya kuukabili mtihani na baada ya hapo husahau Kiswahili. Hili linasababisha wanafunzi ambao hata baada ya kupata alama nzuri katika mtihani bado hawana ujuzi wa kuzungumza sentensi nzima ya Kiswahili sanifu. Hata kama hujaribu huzungumza Kiswahili basi ukizungumza kwa matamshi mabaya ambayo yana athari ya lugha ya kwanza. Hali hi yanaweza kubadilishwa kama wizara ya elimu nchini Kenya itaanzisha utahini wa stadi za kusikiliza na kuongea na walimu kubadilisha mtindo wa kutumia ubao na chaki ambao umepitwa na wakati na kutumia mbinu zinazohusisha wanafunzi katika mazungumzo.

Kwa kuzingatia maoni haya, utafiti huu ulichunguza ufaafu wa matumizi ya mbinu ya majadiliano vikundini kufundishia stadi ya kuzungumza katika shule za upili tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya. Mbinu ya majadiliano ya vikundi ni mojawapo ya mbinu za kisasa inayotumiwa zaidi katika taasisi za elimu ya juu kwa ufanisi mkubwa na ni rahisi kutumiwa pamoja na mbinu zingine za kufundisha.Wanafunzi hugawanywa katika makundi na kupewa mada za kujadiliana ambapo lengo kuu ni kuendeleza mafunzo na mtagusano miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, mara nyingi uboreshaji wa stadi ya kuzungumza hautiliwi maanani katika vikundi hivi vya majadiliano.

**1.3 Suala la Utafiti**

Wanafunzi wengi wanaomaliza shule za upili hukosa umilisi wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.Wengi wao hata huwa na alama nzuri katika mtihani lakini hawana ujuzi wa kuzungumza sentensi nzima ya Kiswahili sanifu ama huzungumza Kiswahili kwa matamshi mabaya ambayo yana athari ya lugha ya kwanza.Hii ni kwa sababu walimu wengi hufunza stadi andishi kwa vile ndizo zinazotahiniwa na kusahau stadi zungumzi kwa vile hazitahiniwi (Babusa 2010).

Kulingana na Kimemia (2001) wanafunzi wengi huwazungumzi lugha ya Kiswahili kwa ufasaha bali hutumia sheng'.Tatizo hili limekita mizizi katika shule zilizo karibu na miji.Sehemu zilizoathirika zaidi ni Kisii na Machakos. Walimu wengi wafundishao Kiswahili pia hutumia mbinu zilizopitwa na wakati za chaki na ubao. Mbinu za kufundishia lugha ya Kiswahili zafaa kuchunguzwa ili kuboresha stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi.

Kulingana na Gathumbi na Masembe (2005) wanafunzi wengi hawazungumzi lugha kwa ufasaha kwa vile walimu hawatilii maanani stadi za kusikiliza na kuzungumza wakati wanapofundisha. Hii inaonyesha kuwa wanafunzi wengi wanaokamilisha masomo ya sekondari hawana umilisi wa lugha. Stadi za kuzungumza na kuongea zinafaa kuzingatiwa sana wakati wa kufundisha lugha kwa vile ndizo stadi za kimsingi.

Lengo kuu la kufundisha lugha ni kuwezesha mwanafunzi kuwasiliana kwa kutumia lugha sanifu na kwa matamshi bora. Utafiti huu ulichunguza ufaafu wa matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza kwa wanafunzi wa shule za upili katika Tarafa ya Moscho, Kaunti ya Kisii, Kenya. Mbinu ya majadiliano ya vikundi ilichaguliwa kwa vile ni mbinu ya kisasa, rahisi kutumia katika ufundishaji na yaweza kutumiwa pamoja na mbinu nyingine za kufundisha.

## 1.4 Lengo la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza ufaafu wa matumzi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi katika kufundisha stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.Utafiti huu pia ulidhamiria kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu tatizo la umilisi wa stadi ya kuzungumza kwa ufasaha miongoni mwa wanafunzi wanaohitimu katika kiwango cha shule za upili.

## 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kama yafuatayo;

i. Kuchunguza matumizi ya majadiliano ya vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza.

ii. Kupambanua shughuli zifanywazo na mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi.

iii. Kuchunguza majukumu ya mwalimu na mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi.

iv. Kutathmini manufaa ya majadiliano ya vikundi kwa wanafunzi.

v. Kuchunguza changamoto zikumbazo majadiliano ya vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza.

**1.6 Maswali ya Utafiti**

Ili kuafikia madhumuni ya utafiti yaliyotajwa, utafiti huu uliibuka na maswali ya utafiti yafuatayo;

i. Je, majadiliano ya vikundi hutumiwa katika kufundshia stadi ya kuzungumza?

ii. Shughuli zipi zilihusishwa katika kufundishia stadi ya kuzungumza?

iii. Majukumu ya mwalimu na mwanafunzi ni yapi katika majadiliano ya vikundi?

iv. Je, majadiliano ya vikundi huwa na manufaa gani kwa mwanafunzi?

v. Changamoto zipi huweza kukumba matumizi ya mbinu ya majadiano ya vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza?

**1.7 Umuhimu wa Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yanaweza kusaidia wizara ya elimu kupitia maafisa wa ubora wa viwango vya elimu ambao wanaweza kupata fahamu kuhusu mbinu mwafaka inayoweza kutumiwa na walimu kuimarisha ufundishaji wa stadi za lugha ikiwemo kuzungumza.Walimu wanaweza kufaidika kwa kutambua mbinu za kutumia ili

kuboresha stadi ya kuzungumza.Wanafunzi pia watafahamu mbinu mpya za kushirikiana katika kusoma pamoja na kuwajibikia kujifunza lugha katika kiwango cha stadi ya kuzungumza. Huu utafiti pia utawafaa watafiti wengine ambao wanaweza kuutumia kama kigezo cha kufanya tafiti za baadaye.

**1.8 Machukulio ya Utafiti**

Utafiti huu unachukulia kuwa:

i. Wasailiwa wangetoa majibu sahihi kwa maswali yote katika hojaji kuhusu matumizi ya majadiliano ya vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza.

ii. Sampuli iliyoteuliwa na kuhusishwa katika utafiti ingewakilisha eneo la utafiti na kuafiki malengo ya utafiti.

**1.9 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulihusisha shule za sekondari katika tarafa ya Mosocho Kaunti ya Kisii kwa vile shule nyingi zimo viungani mwa jiji la Kisii na kulingana na wataalamu wanafunzi wa shule za mijini hawazungumzi Kiswahili fasaha. Utafiti ulihusisha shule sita miongoni mwa shule kumi na tano za upili zilizoteuliwa kupitia sampuli tabakishi. Utafiti huu pia ulihusisha matumizi ya mbinu ya majadiliano katika vikundi na stadi ya kuzungumza tu.

**1.10 Msingi wa Kinadharia**

Kulingana na Yuko na Orien (2005) nadharia ni mfumo wa kuelezea jambo kwa kubainisha vibadala na sheria zinazohusisha vibadala hivi kimoja kwa kingine.

Utafiti huu ulijikita katika nadharia ya majukumu ya Robert Owen ya mwaka 1998 ionyeshayo kuwa watu wana majukumu ya kila mmoja katika shirika. Mahusiano yao

husaidia kuthihirisha majukumu ya kila mtu. Kulingana na nadharia hii, kila mhusika sharti afasiri majukumu yake na ufasiri huu hutegemea nini kila mmoja amechangia katika shirika. Utekelezaji wa majukumu katika shirika aghalabu hutegemea maazimio ya kiongozi wa shirika. Inaaminika kuwa kila mmoja katika hali hii hujaribu kutekeleza wajibu wake kulingana na matakwa ya wengine katika kikundi. Kulingana na Owen, majukumu mahususi ya washiriki katika kikundi hujumuisha mambo yafuatayo;

i. Majukumu ambayo husaidia kikundi kumaliza majukumu yake ni kama vile; kuchangia mawazo, kutafuta habari, kutafuta maoni kutoka katika kikundi, kutoa maoni, kuongoza kikundi ili kuafikia malengo ya kundi.
ii. Ujenzi wa makundi na kuyahifadhi.

Hili jukumu huchangia katika kubuni mazingira mwafaka ya utenda kazi na mshikamano wa wanachama wa kundi husika. Majukumu ya kutenda na kudumisha kundi ni kama vile; kutia moyo wanachama kuangazia shughuli wanayofanya, kusawazisha tofauti miongoni mwa wanachama, kuhimiza wanachama wanyamavu kuzungumza, kuweka kiwango cha hali ya juu cha matokeo.

Kwa kurejelea nadharia hii, majadiliano ya vikundi huhitaji mwalimu kuwa na jukumu la kuongoza wanafunzi kwa kuelekeza tu; wanafunzi ndio wanafanya shughuli darasani (kujadiliana). Mwalimu anafaa kuondoa tofauti miongoni mwa wanafunzi na kusaidia wanafunzi wanyamavu kuzungumza na kubuni mikakati ya kuhakikisha ubora wa ujifunzaji katika vikundi; hali ambayo huchangia ushiriki wa wanafunzi wote na kuweza kuwajibikia shughuli za kundi lao.Wanafunzi

wanyamavu wana nafasi ya kukuza stadi ya kuzungumza kwa vile ujengaji wa vikundi uhakikisha kuwa kuna usawazishaji wa tofauti miongoni mwa wanafunzi. Mshikamano huu huchangia kuafikia malengo ya vikundi. Nadharia hii inafaa kwa utafiti kwa vile inahusiana na vibadala vya utafiti ambavyo ni kigeu huru ambacho ni majadiliano ya vikundi darasani ambapo wanafunzi na walimu huwa na majukumu mbalimbali na kibadala tegemezi uboreshaji wa stadi ya kuzungumza ambapo watu(wanafunzi) wanyamavu wanapata nafasi kuongea jinsi ibainikavyo katika nadharia ya majukumu.


## 1.11 Mhimili wa Dhana ya Utafiti

Mhimili wa dhana ni kielelezo cha mada inayotafitiwa unaoonyesha uhusiano wa vigeu katika utafiti na husaidia mtafiti kuonyesha uwelewaji wake wa swala husika na kuliwasilisha.Mhimili wa dhana humfanya mtafiti kuonyesha uhusiano wa maswala yanayozungumziwa (Kombo na Tromp, 2006).

Kulingana na Mwei (2010), mhimili wa dhana hubaini vigeu vya utafiti. Vigeu huru vinavyotafitiwa, vigeu tegemezi ambavyo matokeo yake hutarajiwa au huathiriwa na vigeu huru na vigeu viingilizi ambavyo huweza kuathiri matokeo ya utafiti lakini aghalabu havitarajiwi.

Utafiti ulihusu matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza .Majadiliano ya vikundi ni mojawapo ya mbinu za kisasa za kufundisha. Mchoro 1 unaonyesha uhusiano wa vigeu huru, vigeu viingilizi na vigeu tegemezi katika utafiti.

**Mchoro 1: Mhimili wa Dhana Ya Utafiti**




Kutokana na mchoro huu,vigeu huru vinahusu matumizi ya majadiliano ya vikundi ambapo majukumu ya mwalimu ni kuandaa mazingira bora ya kufanya shughuli za vikundini na kuwaelekeza wanafunzi. Wanafunzi nao wana jukumu la kukishiriki katika majadiliano na shughuli za vikundini. Wakati wa majadiliano kunaweza kuwa na vigeu viingilizi ambavyo vinaweza kuchangia ama kuathiri matokeo kwa mfano sera ya lugha shuleni, motisha na mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kigeu tegemezi katika utafiti ni umilisi wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

## 1.12 Ufafanuzi wa Istilahi

**Jukumu**

Kile kinahitajika kwa mtu kutokana na mtagusano na wengine au kile anachofaa kufanya katika kikundi. Walimu na wanafunzi huwa na majukumu mahususi katika majadiliano ya vikundi.

**Kutathmini**

Kupima kiwango ambacho mwanafunzi huimarika baada ya kujifunza jambo fulani. Tathmini hufanywa na mwalimu baada ya kufundisha ili kukadiria uwezo wa mwanafunzi katika kuelewa mada fulani.

**Sampuli Tabakishi**

Huu ni mtindo wa kuleta sampuli kwa minajili ya kupata wanafunzi idadi sawa kwa jinsia tofauti. Sampuli hii hugawa sampuli katika vijikundi bainifu kulingana na sifa za kila kikundi kutegemea ukubwa wa makundi makuu. Baadaye kiasi au idadi ya kila tabaka huteuliwa ili kupata sampuli halisi ya kutumiwa katika utafiti.

**Sampuli ya kinasibu**

Kuteua sampuli ya kutumiwa kutoka kwa sampuli lengwa bila mapendeleo yoyote. Katika sampuli hii kila mhusika ana nafasi ya kushirikishwa katika utafiti bora bahati imwangukie.

**Stadi za lugha**

Hivi ni vipengele vya kufundishia lugha. Stadi za lugha ya Kiswahili ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Katika lugha stadi za kusiliza na kuzungumza ndizo za kimsingi.

**Umilisi wa lugha**

Uwezo wa kuelewa na kutumia ujuzi aliopata mtu katika matumizi ya lugha katika mawasiliano. Mtu akiwa na umilisi wa lugha huwa na uwezo wa kuizungumza kwa ukakamavu na ufasaha.

**Vigeu vya utafiti**

Vibadala ambavyo vinaathiri au kuathiriwa na utafiti. Katika utafiti kuna vigeu huru, tegemezi na vigeu vingilizi.

# SURA YA PILI
# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii iliangazia maandishi yanayohusiana mada tafitiwa. Ilihusisha mapitio ya vitabu, majarida, makala na kumbukumbu nyingine zinazohusiana na swala la utafiti na hujihusisha kimahususi na vibadala vya utafiti na hubainisha mianya iliyoachwa na maandishi ya awali kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Maandishi yaliyohakikiwa ni ya sasa na zamani ili kuthibitisha hali iliyopo kuhusu majadiliano ya vikundi na ufundishiji stadi ya kuzungumza. Sehemu hii ilihusisha mambo yafuatayo:

(i) Dhana ya majadiliano katika vikundi na uundaji wa vikundi darasani.

(ii) Shughuli zifanywazo vikundi zinazohusu stadi ya kuzungumza.

(iii) Jukumu la mwalimu na mwanafunzi katika majadiliano katika vikundi.

(iv) Manufaa na ufaafu wa mbinu ya majadiliano ya vikundi.

(v) Changamoto ziwezazo kukabili majadiliano katika vikundi miongoni mwa wanafunzi.

(vi) Muhtasari kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada na ubainishaji wa Mapengo ya kuzibwa na utafiti.

## 2.2 Dhana ya majadiliano ya vikundi na uundaji wa vikundi

Majadiliano ya vikundi ni aina ya ujifunzaji kwa ushirika ambako lengo lake ni kushirikisha wanafunzi wote ili kuwaendeleza kielimu, kubadili mielekeo yao, na kukuza stadi za kuwasiliana na wengine (Kokemuller, 2007). Kulingana na Ohair na


Wiemann (2004) kila mwanafunzi katika kikundi anafaa kupewa nafasi kuongea na kwa sababu hii majadiliano vikundini huwa na urasmi fulani. Hata hivyo vikundi vikiwa na wanafunzi wengi, nafasi ya kuongea huwa finyu na ni wanafunzi wachache hupata nafasi kutoa maoni yao pia mtagusano huweza kukosekana.

Kulingana Creamers (1994) kuuandaa wanafunzi katika vikundi sharti kufanywe ili vikundi hivyo kuchangia matokeo bora. wanafunzi wanaweza kuwekwa katika vikundi vya wanafunzi walio na uwezo sawa au wanaotofatiana.Anapendekeza kuwe na vikundi ambavyo wanafunzi wana uwezo tofauti kushirikiana.

Kulingana na Bennet na Dunne (1992) katika uundaji wa vikundi sharti mwalimu atafute njia mwafaka ya kuviunda. Kwa maoni yake wanafunzi wanafaa wawe kati ya wanne na sita katika kikundi ili waweze kujadiliana vyema na kutumia vifaa kwa njia nzuri.

Kulingana na Kagan (1988) uundaji wa vikundi na idadi ya wanafunzi katika kikundi ni muhimu na huweza kuathiri mtagusano na mawasiliano miongoni mwao. Anadokeza kuwa idadi ya ya wanafunzi hadi watano katika kikundi ni sawa. Ameonyesha hali hii katika mchoro 2.1 unaodhihirisha kuwa mawasiliano katika kundi la wanafunzi watatu hadi wanne unafaa. Kundi kubwa huweza kufanya wanafunzi kuwa na vikundi vidogo vidogo vinavyoweza kusambaratisha shughuli za vikundi na kutatiza mawasiliano vikundini.

**Mchoro 2: Mawasiliano katika vikundi**



**Wanafunzi watatu**　**Wanafunzi wanne**　**Wanafunzi watano**

Katika kupanga wanafunzi vikundini, wanafunzi wanaweza kuchaguana ama mwalimu mwenyewe kuwapanga wanafunzi katika vikundi kulingana na uwezo wao. Katika kuandaa shughuli za kufanywa vikundini, mwalimu anafaa kuandaa maswali yanayoshughulikiwa mapema. Maswali haya yanaweza kuandikwa ubaoni wanafunzi wayanakili. Mbali na shughuli ya kufanywa lazima vifaa pia viandaliwe. Baada ya kufanya hayo wanafunzi wawe katika vikundi wakishughulikia maswali yaliyomo katika nakala ya maswali. Katika kila kikundi kuwe na mwenyekiti atakayeongoza kikundi na katibu ambaye ataandika mambo muhimu yanayojadiliwa kikundini. Mwenyekiti atahakikisha majadiliano yanaendeshwa kwa njia ifaayo. Wanafunzi wakiwa katika vikundi wakijadiliana,mwalimu apite akikagua kuwa kila mwanafunzi anashiriki kwa kutoa maoni na kuhakikisha kuwa yote yanayojadiliwa yananakiliwa ili kuwasilishwa baadaye katika kikao kitakachoandaliwa na mwalimu. Maoni haya pia yametolewa na (Clark, 1971) anapodokeza kuwa vikundi vya majadiliano vinafaa kuongozwa na wanafunzi kwa zamu na mwalimu awe na imani kwa wanafunzi kuwa wana uwezo wa kujiongoza wenyewe.

**2.3 Shughuli zifanywazo vikundini zihusianazo na stadi ya kuzungumza**

Kulingana na Ndalu (1997) shughuli zinazofanywa vikundi zinazohusiana na stadi ya kuzungumza ni kama; kukariri mashairi, kuimba nyimbo, kuigiza, kutamba hadithi,

dayolojia na kuchambua makala. wanafunzi wanapofanya shughuli vikundini mwalimu anafaa kukadiria na kutathmini kazi yao kwa kuandaa maswali ya kukadiria umilisi wa stadi mbalmbali kama vile; kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza (Richards na Rodgers, 2001).

Kuna mambo mengi yanayoziangatiwa wakati wa kutathmini stadi ya kuzungumza katika majadiliano ya vikundi kama vile; kusoma maneno kwa sauti, kukamilisha sentensi, kutafsiri kifungu cha maneno, kuelezea kuhusu uraibu, mahojiano kati ya wanafunzi wawili au zaidi, uigizaji wa maongezi ya watu wengine, uwasilishaji wa hoja mbele ya wanafunzi wengine,kusimulia kisa kifupi na kuelezea kuhusu mchoro na ramani mingoni mwa mengine.

Kulingana na Ndalu (1997) vipengele vya shughli ya kutathmini stadi ya kuzungumza ni; utamkaji bora wa maneno na ufasaha wa kuongea, uzingatiaji wa alama za uakifishaji, namna mwanafunzi anashirikiana na wengine, uelewaji wa maagizo na uwezo wa kusimulia kisa upya baada ya kusoma au kusimuliwa.

## 2.4 Majukumu ya mwalimu na mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi.

### 2.4.1 Majukumu ya mwalimu katika majadiliano ya vikundi

Mwalimu ana majukumu kadhaa katika mijadala ya vikundi. Anafaa kuandaa shughuli za vikundini, kutafuta vifaa vya kutosha wanafunzi katika vikundi vyao, kuandaa kipindi cha wanafunzi kuwasilisha hoja zao kisha atoe mtazamo wake na kugusia mambo muhimu. Mwalimu pia anafaa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanadumisha nidhamu, kuwapa nafasi kutoa maoni, kuwaelekeza kuhusu maswala

ibuka, kukadiria muda unavyotumiwa wakati wa majadiliano vikundini na kuwatathmini.

Kulingana na Clark (1971) mwalimu ni mtaalamu ambaye anawaongoza wanafunzi kukua watu wazima na kuweza kuelewa shida zinazowakumba katika mazingira yao na anaweza kuhusishwa katika mjadala iwapo wanafunzi watahitaji usaidizi. Mwalimu pia anafaa kuwa na imani kuwa wanafunzi wanaweza kujisimamia wanapojadiliana vikundini.Maoni kama haya pia yametolewa na Lembo (1972) ambaye anaona mwalimu kama mwelekezi anayeweza kuandaa mazingira ya kujifunza kupitia mijadala ya vikundi, kuchagua vikundi, kuwapa wanafunzi vifaa na maswali ya kushughulikia na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki, kuandaa malengo ya somo na kuwapa wanafunzi muda wa kumalizia shughuli zao na pia kuongezea hoja na kurekebisha makosa kutokana na wasilisho la mwanafunzi. Klingana na Brown (2007) mwalimu anafaa kubuni mazingira darasani ya kuhimiza wanafunzi kujaribu kutumia lugha kwa kutoa maoni yao na kuhakikisha shughuli zinafanywa na wanafunzi ni rahisi kwa kutumia mtindo unaoeleweka na wanafunzi.

### 2.4.2 Majukumu ya mwanafunzi katika majadiliano ya vikundi

Kulingana na Lembo (1972) wanafunzi wanasoma vyema wanaposhiriki, wakichagua mwelekeo wao,kugundua maswala yao, na kuamua namna wanavyosoma na kushikamana na matokeo na athari ya uchaguzi wao. Wanafunzi pia anafaa kuhusishwa katika uundaji wa vikundi ambapo watachagua mwenyekiti wa kuongoza kikundi na katibu wa kunakili hoja zitakazowasilishwa katika mijadala. Katika hali hii kila mwanafunzi anahitajika kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yake. Maoni

kama hayo pia yametlewa na Clark (1971) aliyesema kuwa majadiliano yanafaa kuongozwa na wanafunzi huku mwalimu akiwa mwelekezi.

**2.5 Manufaa ya Majadiliano ya Vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza**

Kulingana na Galanes & Adams (2013) mwananafunzi katika kikundi anaweza kuyafanya yale hawezi kufanya akiwa peke yake pia husaidia mwanafunzi kuzungumza na wengine na kuimarika kielimu kwa kujadiliana, kueleza aliyonayo na kuchangia katika ujifunzaji wake kwa kutoa maoni na kuyathibitisha. Mawazo hayo yamepingwa na O'hair & Wiemann (2004) waliodokeza kuwa majadiliano ya vikundi hayawapi wanafunzi wote nafasi kutoa maoni hasa katika vikundi vikubwa. Kila mmoja katika kikundi hutaka kuongea. Hali hii huleta ufinyu wa muda.

Kulingana na Brown (2007) wanafunzi katika vikundi wanasaidiana kupokezana habari muhimu kama 'timu' ambayo washiriki wake hufanya kazi pamoja kufikia malengo yao . Mbinu hii husaidia katika kukumbuka mambo kwa muda mrefu na huwapa wanafunzi nafasi kuwajibiki.

Bromfit (1991) akirejerea mradi wa kufundisha wanafunzi wajerumani Kiingereza katika mwaka 1970-1972 anaeleza kuwa wakati wanafunzi wanafundishwa katika vikundi vidogo, wanatagusana na hivyo kuwa na umilisi wa lugha kutokana na kushirikiana na kuchangiana mawazo. Brumfit katika muktadha huu hajaonyesha shughuli zinazohusishwa katika majadiliano vikundini kuboresha umilisi wa lugha.

Uwezo wa kuwasiliana vyema katika miktadha mbalimbali ndilo lengo kuu la majadiliano ya vikundi darasani( Bachman,1990). Maoni haya yanashabihiana na

Barbara (1993) aliyesema kuwa wanafunzi wanapokuwa vikundini hufanya juhudi kuwasiliana na wengine hivyo kuimarisha kiwango cha kutumia lugha.

Kulingana na Vigotsky (1978) wanafunzi huwa na uwezo wa kufanya vyema zaida wakiwa katika vikundi kuliko wakiwa peke yao. Majadiliano ya vikundi huchangia pakubwa katika mafunzo ya kiwango cha juu miongoni mwa wanafunzi. Maoni kama haya yalitolewa na Geoffrey (1993) akidokeza kuwa majadiliano ya vikundi huimarisha stadi ya mawasiliano na kupatia wanafunzi nafasi kutumia msamiati waliofunzwa.

Katika nchi ya Marekani, tafiti nyingi zinaonyesha kuwa kusoma katika vikundi huchangia matokeo bora, uhusiano mwema wa kijinsia na mielekeo chanya miongoni mwa wanafunzi. Utafiti kuhusu matumizi ya majadiliano ya vikundi kufundishia lugha na Hesabu ulionyesha kuwa matokeo ya mtihani wa wanafunzi waliohusishwa katika vikundi yaliimarika ikilinganishwa na kundi la wanafunzi wasiokuwa vikundini ( Dunne, 1990).

Waandishi waliorejelewa wamebainisha wazi manufaa ya majadiliano ya vikundi hata hivyo hawakuonyesha jinsi mbinu ya majadiliano ya vikundi itatumiwa kufundishia stadi ya kuzungumza. Maelezo yao mengi ni ya jumla tu kuhusu umuhimu wa majadiliano ya vikundi pia hawakudhihirisha shughuli katika vikundi ambazo zitaendeleza stadi ya kuzungumza. Maandishi yaliyorejelewa yanajikita katika nchi za kigeni kama vile; Ujerumani, Marekani na nchi nyinginezo. Utafiti huu ulidhamiria kuziba pengo hili na kuibuka na mitamo mipya katika mazingira halisi

kwa kuchunguza uhusiano wa majadiliano ya vikundi na stadi ya kuzungumza katika shule za upili tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.

## 2.6 Changamoto Zikabilizo Majadiliano Katika Vikundi

Kulingana na Galanes na Adams (2013) changamoto kuu katika majadiliano ya vikundi ni kuwa si wanafunzi wote watapata nafasi kushiriki kuongea na kutoa maoni yao. Kuna urasmi mwingi katika majadiliano ya vikundi na kila mmoja hutafuta kibali kutoa maoni hali inayoweza kufungia nje wanafunzi wengi.

Dunne na Bennet (1990) wamedokeza changamoto zifuatazo zinazoweza kubabili majadiliano katika vikundi miongoni mwa wanafunzi;

(i) Wanafunzi wazembe wanaweza kujificha katika kikundi bila kushiriki.

(ii) Muda unaweza kuwa kikwazo iwapo shughuli za vikundi hazimaliziki.

(iii) Mbinu hii inahitaji nafasi kubwa na vifaa vya kutosha.

(iv) Wanafunzi wanaweza kukosa hamu ya kutaka kufanya kazi ya vikundi.

(v) Kunaweza kuzuka tofauti za kimaoni miongoni mwa wanafunzi vikundi.

## 2.7 Muhtasari wa yaliyoandikwa kuhusu mada na pengo la utafiti

Sura hii imeangazia dhana ya majadiliano katika vikundi, uundaji wa vikundi, umuhimu wa mbinu ya majadiliano katika vikundi, majukumu ya mwalimu na wanafunzi shughuli zifanywazo vikundini na utathmini wa wanafunzi katika vikundi. Mchango wa waandishi mbali mbali umechanganuliwa kudhihirisha dhana ya majadiliano katika vikundi.

Pengo lililopo hata hivyo ni kuwa waandishi wengi walioshughulikia mbinu hii wametoka nchi kama Marekani na nchi za Ulaya na maelezo mengi yanajikita katika

mazingira yao.Waandishi wengi wameshughulikia matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi kijumla. Wengi waohawakudhihirisha jinsi majadiliano katika vikundi yataimarisha stadi mbalimbali za lugha ikiwemo stadi ya kuzungumza.Utafiti huu ulidhamiria kuziba mapengo katika maandishi hayo na kuibuka na uelewaji mpya kuhusu matumizi ya mbinu hii ya majadiliano ya vikundi. Utafiti ulichunguza ufaafu wa mbinu hii katika kufundishia stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.

# SURA YA TATU
# MBINU ZA UTAFITI.

## 3.1 Utangulizi

Sura hii ilidhamiria kuelezea mbinu za utafiti zilizotumiwa katika kufanya utafiti huu. Inahusisha maelezo kuhusu muundo wa utafiti, wasailiwa walengwa ,mahali pa kufanyia utafiti, sampuli na mchakato wa uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, ukusanyaji data na uchanganuzi wa data.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni utaratibu unaofuatwa ili kupata majibu kwa maswali ya utafiti (Orodho, 2003). Kulingana na Kombo na Tromp (2006) muundo wa utafiti huwa ni mfumo ambao hulenga kujibu maswala katika utafiti. Kupitia kwa muundo wa utafiti, mtafiti huzua maswali yatoayo habari inayohitajika pia hufafanua walengwa na jinsi utafiti utafanywa. Muundo wa utafiti hutoa mwelekeo kuhusu ukusanyaji data na uchanganuzi wake (Kothari, 2011).

Muundo uliotumiwa katika utafiti huu wa majaribio. Muundo majaribio ulifaa katika utafiti huu kwa sababu kulikuwa na makundi mawili ya wanafunzi katika kila shule iliyohusishwa katika utafiti; kundi moja ndilo lilihusishwa katika jaribio la utafiti ilhali kundi la pili halikuhusishwa. Makundi yote yalihusishwa katika mtihani wa kwanza na wa mwisho baada ya utafiti. Muundo huu ulisaidia kupata majibu ya maswali ya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu ya majadiliano katika vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.

### 3.3 Mahali pa Kufanyia Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika tarafa ya Mosocho, wilaya ya Kisii ya Kati. Tarafa hii ni miongoni mwa tarafa sita zinazounda wilaya ya Kisii ya kati nazo ni; Mosocho, Marani, Getembe, Keumbu, Kiogoro na Kegogi. Tarafa hii inapakana na mji wa Kisii na ina shule kumi na tano zikiwemo kumi za kutwa na tano za bweni .Utafiti ulifanywa katika wilaya ya Kisii hasa Tarafa ya Mosocho kwa vile ni eneo ambalo utafiti wa awali ulidhihirisha kuwa na tatizo la wanafunzi kutumia lugha ya Sheng'hivyo basi kukosa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

### 3.4 Walengwa

Walimu wawili wanaofundisha Kiswahli kutoka kila shule iliyoteuliwa katika Tarafa ya Mosocho walihusishwa katika utafiti. Jumla ya walimu kumi na wawili walishirikishwa katika utafiti. Walimu wakuu pia walihusishwa katika utafiti; hasa walio katika shule zilizoteuliwa kwa vile wao ndio wasimamizi wa mtaala shuleni na kutoa kibali cha kufanya utafiti shuleni. Utafiti huu pia ulihusisha wanafunzi mia nne themanini kutoka shule zilioteuliwa ili kushirikishwa katika utafiti.

### 3.5 Sampuli na Mchakato wa Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulihusisha shule sita za upili katika tarafa ya Mosocho. Shule hizi ziliteuliwa kulingana na viwangovya shule za bweni na za kutwa kwa kutumia sampuli tabakishi ili kuhakikisha kila kundi lilihusishwa katika sampuli lengwa. sampuli makusudi ilitumiwa kuteua madarasa yaliyotumiwa katika utafiti na kila darasa kuwa na wanafunzi takribani arobaini. Walimu wakuu sita na walimu kumi na wawili wafundishao somo la Kiwsahili waliteuliwa kwa kutumia sampuli makusudi.

Kulingana na Kombo &Tromp (2006) sampuli makusudi uhusu uchaguzi wa makundi mahususi yanayobainika mapema. Jedwali 3.1 linadhihirisha uteuzi wa sampuli.

**Jedwali 3.1 Uteuzi wa sampuli.**

| Shule | Idadi | % | wanafunzi | % | walimu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shule za bweni | 2 | 33.3 | 320 | 66.7 | 4 | 33.3 |
| Shule za kutwa | 4 | 66.7 | 160 | 33.3 | 8 | 66.7 |
| Jumla | 6 | 100 | 480 | 100 | 12 | 100 |

## 3.6. Vifaa Vya Kukusanya Data

Utafiti huu ulitumia vifaa vya ukusanyaji data vifuatavyo;

### 3.6.1 Mtihani mwanzoni na mwishoni mwa utafiti

Kulikuwa na vikundi viwili; kimoja kilihusishwa katika utafiti na kingine hakikuhusishwa lakini vikundi vyote vilihusishwa katika mtihani wa kwanza

na mwisho. Mtihani wa kwanza ulifanywa mwanzoni mwa ilhali wa pili ulifanywa baada ya miezi miwili baada yawanafunzi walioteuliwa kushirikishwa katika majadiliano vikundini. Sampuli makusudi ilitumiwa kugawa madarasa katika makundi mawili kwa kutumia orodha ya majina ya kila darasa.

Wanafunzi wote waliohusishwa ni 229 miongoni mwa wanafunzi 480 katika shule sita zilizoteuliwa. Kila darasa litagagwanywa katika vikundi viwili; kundi la kwanza lilihusishwa katika majadiliano ya vikundi na la pili halikuhusishwa. Makundi yote mawili yalihusishwa katika mitihani yote miwili ili kuchunguza uhusiano kati ya majadiliano ya vikundi na stadi ya kuzungumza.

### 3.6.2 Hojaji

Kulingana na Wamitila (2003) hojaji ni hati yenye orodha ya maswali ambayo humwongoza mtafiti katika utafiti. Maswali hayo hulenga masuala mbalimbali kuhusiana na anayehojiwa. Kuna hojaji wazi ambapo mhojiwa hutoa majibu ya kina na hojaji funge ambapo mhojiwa hujikita kwenye maswali yaliyoulizwa tu na kuchagua mojawapo ya majibu. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) hojaji ni muhimu katika kukusanya data kwa vile ni rahisi kutumia na si ghali sana na inaweza kutumiwa kwa sampuli kubwa. Hojaji zilitumwa kwa wanafunzi wote mia nne themanini katika shule sita zilizoteuliwa na walimu kumi na wawili wafundishao Kiswahili katika shule zilizoteuliwa ili kupata maelezo yao kuhusu matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi katika kufundishia stadi ya kuzungumza**.**

### 3.7. Majaribio Ya Vifaa Vya Utafiti

Kulingana na Wiersman (1985) majaribio ya utafiti hubainisha udhaifu wa vifaa vya utafiti na kurekebisha makosa yaliyomo kabla ya kuvitumia katika utafiti wenyewe. Majaribio hayo pia hudhihirisha uhalali na utumainifu wa vifaa hivyo. Majaribio hayo yalifanywa katika shule mbili za upili katika tarafa ya Mosocho ambazo hazitashirikishwa katika utafiti.

### 3.7.1 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti

Kulingana na Orodho (2005) uhalali ni kiwango ambacho vifaa vya utafiti vinatumika inavyofaa.Vifaa hivi sharti vichunguzwe uhalali wao kabla ya kutumiwa katika utafiti kamili. Swala kuu la kuzingatia ni uhalali wa vifaa hivyo katika mada husika. Majaribio yalifanyiwa vifaa vya utafti ili kukadiria uhalali ili kuhakikisha maswali

yaliyolenga mada. Uhalali pia ulitathmini kiwango cha lugha katika hojaji na kuhakikisha kuwa vigeu vyote vilihusishwa katika hojaji. Jedwali sailifu lilitumiwa kuchunguza ufaavu wa maswali yaliyokuwa katika hojaji. Wasimamizi wangu pia walichunguza uhalali wa maswali yaliyokuwa katika hojaji. Baadaye hojaji sahihi ilitayarishwa kutumika katika ukusanyaji wa data nyanjani.

### 3.7.2 Utumainifu wa Vifaa vya Utafiti

Utumainifu wa vifaa ni kiasi ambacho vifaa vya utafiti vinaweza kuleta matokeo yaleyale vinapotumiwa mara kadha (Orodho, 2005). Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) utumainifu ni kiwango ambacho vifaa vya utafiti vinazalisha matokeo yanayotegemewa kila wakati vinapotumiwa. Mbinu ya majaribio ya kurudiwa hutumiwa kwa kundi husika kukiwa na mpito wa wakati baina ya jaribio la kwanza na la pili. Kipimo cha Pearson kinaruhusu kiwango kati ya 0.5 na 1, (Ingule na Gatumu, 1996).

Katika kuhakikisha utumainifu, majaribio yalifanywa kwa kurudiwa katika shule mbili katika Tarafa ya Mosocho ambazo hazikuhusishwa katika utafiti kamili. Matokeo ya majaribio katika kipimo cha uwiano yalikuwa $r=0.73$ kiwango ambacho kiliweza kutegemewa katika kufanya utafiti.

## 3.8 Utaratibu Wa Kukusanya Data

Kabla ya kuanza kukusanya data, mtafiti alipata kibali cha utafiti kutoka kwa Kamati ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Mtafiti pia alipata kibali kutoka kwa wakuu wa shule sita husishwa. Maswali ya mitihani yalitumwa kwa walimu walioteuliwa kutahini wanafunzi kabla na baada ya kutumia mbinu ya

mijadala ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza . Matokeo ya mitihani hiyo yalirekodiwa na kulinganishwa ili kuchunguza uhusiano kati ya majadiliano ya vikundi na stadi ya kuzungumza. Hojaji zilitumwa zikiambatanishwa na barua za utangulizi ambazo zilionyesha mada, lengo la utafiti na muda wa kutumiwa katika utafiti. Baada ya kupata kibali cha kufanya utafiti katika shule zilizoteuliwa, walimu waliombwa kuwasilisha orodha ya majina ya wanafunzi waliohusishwa katika utafiti.

### 3.9 Uchanganuzi wa Data

Kulingana na Kombo na Tromp (2006), uchanganuzi wa data humaanisha uchunguzi wa data iliyokusanywa na kufanya uchakataji na kutolea maelezo. Uchanganuzi wa data kutokana na hojaji na mitihani ulifanywa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Data kutokana na hojaji ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya tarakilishi ya SPSS baada ya kuitenganisha katika vijisehemu kama zilivyohusiana na data nzima ili kuonyesha uhusiano kati ya matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi na umilisi wa stadi ya kuzungumza. Data iliyohusu madhumuni ya kwanza, pili, tatu na tano yalichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya tarakilishi ya SPSS baada ya kugawanywa visehemu na kuzalisha tarakimu na asilimia. Madhumni ya nne yalichanganuliwa kutokana data ya hojaji na mtihani wa kwanza na mwisho.

Data kutokana na hojaji ilichanganuliwa kwa SPSS na matokeo ya mtihani wa mwanzo na mwisho yalilinganishwa kwa kutumia vipimo vya mielekeo ya ukatikati kama cha wastani na umbali kuonyesha mtawanyiko wa alama kati ya kundi husishwa na lisilohusishwa katika utafiti kabla na baada ya matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi vilevile kipimo cha uwiano cha spearman kilitumiwa ili kukadiria

uhusiano baina ya kigeu huru (matumizi ya majadiliano ya vikundi) na kigeu tegemezi (umilisi wa stadi ya kuzungumza). Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa katika chati na majedwali na kujadiliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Hitimisho na mapendekezo yalitolewa kutokana na data iliyochanganuliwa kwa manufaa ya walimu, wanafunzi maafisa wa kukadiria ubora wa elimu (QASO) na watafiti wengine kwa manufaa ya utafiti wa baadaye.

### 3.10 Swala la maadili

Kabla ya kufanya utafiti, barua ya utambulishi ilitolewa na Chuo kikuu cha Kenyatta iliyosaidia kupata kibali cha utafiti kutoka Kamati ya Kitaifa ya Sayansi,Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Barua za kibali zilitumwa kwa wakuu wa shule.Utafiti ulifanywa kwa uwazi na uaminifu na data iliyokusanywa ilikuwa sahihi. Matokeo ya mitihani na maoni yaliyopokewa kutoka kwa wasailiwa yaliheshimiwa na yalitumiwa tu kwa ajili ya utafiti wala hayakufichuliwa kwa mtu mwingine.

Wizi wa kitaaluma ni kinyume na uandishi wa kimaadili. Kulingana na Mligo (2012) wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa maneno, mawazo, au vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti au watu wengine bila kuonyesha ni ya nani na chanzo chake. Utafiti huu uliepukana na wizi wa kitaaluma kwa kutambua mchango wa waandishi wengine na vyanzo vyote vya mawazo yao kwa kufanya unukuzi sahihi wa maandishi yao.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA DATA,UCHAMBUZI NA MAELEZO

## 4.1 Utangulizi

Sehemu hii ilihusisha uwasilishaji wa data iliyokusanywa nyanjani, uchambuzi wa data na maelezo kutokana na data iliyochanganuliwa. Sehemu ya kwanza ilishughulikia wasailiwa, maelezo yao ya kibinafsi, utumainifu na ukadiriaji wa ufaafu wa data. Mbinu za uchanganuzi wa data zilitumiwa kuchanganua data, kuiwasilisha na kutolea maelezo kulingana na madhumuni ya utafiti.

## 4.2 Wasailiwa walengwa

Sampuli lengwa ilihusisha wasailiwa 492, iliyojumuisha wanafunzi 480 na walimu 12. Wasailiwa wote walioteuliwa walipatikana na kushiriki katika kujaza hojaji zikarudishwa na walimu walioteuliwa. Idadi hii iliwakilisha asilimia mia moja ya wasailiwa inavyobainika katika jedwali 4.1.

**Jedwali 4.1 Idadi ya wasailisiwa wanafunzi na walimu.**

| Idadi | Walimu washirikishwa | Wanafunzi washirikishwa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Idadi lengwa | 12 | 480 | 492 |
| Walioshiriki | 12 | 480 | 492 |
| Jumla asilimia (%) | 100 | 100 | 100 |

Kutokana na jedwali 4.1, inadhihirika kwamba wasailiwa wote walishiriki kujaza hojaji. Hili ni dhhirisho kuwa data iliweza kutumika kwa hakika kupimia matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii,

Kenya.Wafuatao ni wanafunzi wote walengwa katika utafiti huu kulingana na aina ya shule.

**Jedwali 4.2 Wanafunzi wasailiwa**

| Kiwango cha shule | Idadi teuliwa | Asilimia(% ) |
|---|---|---|
| Shule za bweni | 320 | 66.7 |
| Shule za kutwa | 160 | 33.3 |
| Jumla | 480 | 100 |

Miongoni mwa wanafunzi teuliwa 480, sampuli makusudi ya wanafunzi 229 iliteuliwa kufanya mtihanni wa mwanzo na wa mwisho katika shule sita teuliwa. Katika sampuli hii kila darasa liligawanywa katika makundi mawli kwa kutumia sampuli ya kinasibu.Wanafunzi 115 katika shule zilizoteuliwa waliteuliwa na kuhusishwa katika majadiliano vikundini ilhali waliobaki 114 hawakuhusishwa katika majadiliano vikundini lakini walifanya mitihani yote miwili. Wanafunzi waliobaki 251 walishiriki katika kujaza hojaji pamoja na 229 waliofanya mtihani.

Wasailiwa waliulizwa waonyeshe jinsia yao.Wanafunzi waliosailiwa, 267 ni wa kiume ilhali 213 walikuwa wa kike kama inavyodhihirika katika jedwali 4.3. Kutokana na data ilidhirika kuwa wanafunzi wa kiume ni wengi kuliko wenzao wa kike. Miongoni mwa walimu waliosailiwa, 8 ni wa kiume ilhali 4 ni wa kike. Ilibainika kukaribia kwa na usawa wa kijinsia mingoni mwa wanafunzi wasailiwa. Madhumuni ya utafiti ni kuchunguza matumizi ya majadiliano ya vikundi, kuchunguza manufaa na changamoto katika shule za wasichana na wavulana.Tatizo la umilisi wa stadi ya kungumza huweza kuathiri jinsia zote.

Kwa upande wa walimu, hakukuwa na usawa wa kijinsia kwa vile walimu wa kike ni wachache mno kulingana na takwimu zilizotokana na utafiti. Walimu ni vielelezo bora kwa wanafunzi katika kukuza stadi zote za lugha ikiwemo stadi ya kuzungumza. Walimu wakiwa na ufasaha wa lugha, wanafunzi watawaiga na hivyo kukuza stadi ya kuzungumza. Walimu pia huwa na jukumu kuwapa wanafunzi motisha na kuwaelekeza na kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za vikundini.

**Jedwali 4.3 Jinsia wanafunzi na walimu**

| Jinsia | Idadi wanafunzi | Asilimia ( %) | Idadi walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Kiume | 267 | 55.6 | 8 | 66.7 |
| Kike | 213 | 44.4 | 4 | 33.3 |
| Jumla | 480 | 100 | 12 | 100 |

Wanafunzi wasailiwa waliulizwa kidato chao na maelezo yao yakawasilishwa katika jedwali 4.4. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba asilimia 37.1% ya wanafunzi wako katika kidato cha kwanza, asilimia 25.4% wako katika kidato cha pili, asimilia 20.8% wako katika kidato cha tatu, asimilia 16.7% wako katika kidato cha nne. Hii ilidhihirisha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili walihusika katika utafiti. Hii data ni ya kutia moyo kwa vile wanafunzi wa kidato cha kwanza na pili wana muda mrefu katika shule na hivyo wangenufaika na umuhimu ambao ungetokana na matokeo ya utafiti.

**Jedwali 4.4: Kidato cha mwanafunzi**

| Kidato cha mwanafunzi | Idadi ya wanafunzi | Asilimia ( %) |
|---|---|---|
| Kdato cha kwanza | 178 | 37.08 |
| Kidato cha pili | 122 | 25.42 |
| Kidato cha tatu | 100 | 20.83 |
| Kidato cha nne | 80 | 16.67 |
| Jumla | 480 | 100 |

Walimu walisailiwa kuhusu viwango vyao vya masomo na maelezo yao yakanakiliwa katika jedwali 4.5. Ilidhihirika kuwa, asilimia 91.7% ya walimu wako na shahada ya digrii, hali asilimia 8.3% ya walimu walikuwa na shahada ya diploma. Walimu wengi walikuwa na shahada ya digrii hivyo huweza kuwa na uwezo zaidi wa kufundisha lugha.

Kulingana na Kimemia(2001) walimu ni kiungo muhimu katika ufundishaji wa lugha na sharti wao wenyewe wapende Kiswahili na kuwa wabunifu wanapofundisha. Mwalimu wa Kiswahili basi lazima asaidie walimu wengine Walimu walioandaliwa vyema huendeleza matumizi bora ya Kiswahili katika mazingira ya shuleni na jamii inayozingira shule.

**Jedwali 4.5 Kiwango cha masomo cha walimu**

| Kiwango cha masomo | Idadi ya walimu | Asilimia(%) |
|---|---|---|
| Digrii | 11 | 91.7 |
| Diploma | 1 | 8.3 |
| Jumla | 12 | 100 |

Wasailiwa waliulizwa kuhusu shule wanayatoka na kutokana na data iliyokusanywa kuptia hojaji zilizotumwa kwao maelezo yao yaliwasilishwa katika jedwali lifutalo;

**Jedwali 4.6 Maelezo ya wanafunzi na walimu kuhusu aina ya shule**

| Aina ya shule | Idadi wanafunzi | Asilimia (%) | Idadi walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Kutwa | 160 | 33.3 | 8 | 66.7 |
| Bweni | 320 | 66.7 | 4 | 33.3 |
| Jumla | 480 | 100 | 12 | 100 |

Kulingana na jedwali 4.6 asilimia 66.7% ya wanafunzi wako katika shule za Bweni na asilimia 33.3% wako katika shule za Kutwa. Kwa upande wa walimu, asilimia 66.7% ya waalimu walikuwa wakifundisha katika shule za Kutwa na asilimia 33.3% walikuwa wakifunza katika shule za Bweni. Dhihirisho ni kuwa shule nyingi katika eneo hili ni za kutwa.

Hii inamaanisha wanafunzi wengi wanaweza kukosa ufasaha wa lugha kutokana na athari za mazingira ya nyumbani ama mtaani ambapo lugha ya Sheng' huzungumzwa. Hii data ni muhimu kwa vile ilisawiri taswira kuhusu baadhi ya changamoto zilizokumba baadhi ya wanafunzi. Wanafunzi wa shule za kutwa huwa na muda mfupi kutagusana na walimu ilhali wale wa shule za bweni huwa na walimu jioni na wikendi. Hali hii huweza kuchangia wanafunzi wa shule za bweni kukuza stadi ya kuzungumza hata kama hawakuhusishwa katika majadiliano ya vikundi. Wanafunzi wa shule za kutwa kwa upande mwingine huenda wakaathiriwa na matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili mitaani na nyumbani.

### 4.3 Maelezo ya wanafunzi kuhusu majadiliano katika vikundi shuleni

Walengwa katika utafiti huu walikuwa wanafunzi na walimu ambao walitumiwa ili kutathmini matumizi ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Kutokana na hojaji zilizowasilishwa kwa wanafunzi, walihitajika kueleza kuhusu kuwepo kwa majadiliano ya vikundi shuleni. Kutokana na hajaji hizo maoni yao yalikusanywa na kunakiliwa katika jedwali 4.7.


**Jedwali 4.7 Maelezo ya wanafunzi kuhusu majadiliano ya vikundi.**

| Majadiliano vikundini | Idadi | Asimilia (%) |
|---|---|---|
| Ndio | *418* | 87 |
| La | *62* | *13* |
| Jumla | *480* | *100* |

Matokeo ya utafiti kutokana na jedwali 4.7 yaonyesha kuwa, asilimia 87% ya wanafunzi walikubali kuwa na vikundi vya majadiliano, hali asilimia 13% ya wanafunzi hawakuwa na vikundi vya majadiliano. Maelezo haya ya wanafunzi yalioonyesha kuwa walimu wanatumia majadiliano ya vikundi shuleni.

Inafaa wanafunzi waelewe jinsi ya kujiandaa vyema kushiriki katika majadiliano vikundini na kushiriki katika utaratibu na uongozi wa vikundi ili kunufaika na majadiliano. Wanafaa kudumisha nidhamu wakati wa majadiliano ya vikundi, kuepukana na mizozo inayoweza kuathiri majadiliano vikundini. Walimu huwa na jukumu la kuelekeza wanafunzi vikundini.

Walimu ni kiungo muhimu katika kufanikisha mtaala shuleni .walimu hutumia mbinu nyingi za kufundishia lugha ya Kiswahili. Kutokana na hojaji walimu waliulizwa kama walitumi mbinu ya majadiliano katika vikundi darasani na maoni yao yakanakiliwa katika mchoro 3.



**Mchoro 3: Chati inayoonyesha maelezo ya walimu kuhusu majadiliano vikundini**

Kulingana na mchoro 3, utafiti waonyesha kwamba asilimia 75% ya waalimu walikubali wana vikundi vya majadiliano katika shule zao, na asilimia 25% walikanusha kwamba hawana vikundi vya majadiliano katika shule zao. Maelezo hayo yalidhihirisha kwamba kuna baadhi ya shule zinakosa kunufaika vikundi vya majadiliano lakini shule nyingi huhusisha wanafunzi katika majadiliano katika vikundi.

Maelezo ya walimu yanaonyesha kuwa huenda ikawa baadhi ya walimu hawaelewi umuhimu wa majadiliano ya vikundi, huwa na mitazamo hasi kuhusu matumizi ya majadiliano vikundini ama hawakutayarishwa vyema wakiwa vyuoni(Kimemia, 2001).

Kwa kiasi kikubwa matokeo ya utafiti pia yanaoana na maoni Babusa (2010) kuwa baadhi ya walimu wanazidi kutumia mbinu zilizopitwa na wakati za chaki na ubao kufundishia stadi za lugha na kuhimiza kuwa walimu sharti wafundishe stadi zote za lugha kwa kutumia mbinu za kisasa ili kukuza uwezo na ukakamavu wa mwanafunzi katika stadi ya kuzungumza kwa ufasaha.

## 4.4 Shughuli zihusishwazo katika kufundishia stadi ya kuzugumza vikundini katika muktadha wa majadiliano ya vikundi

Utafiti huu ulibainisha kuwa shughuli zifanywazo vikundini ndizo hutumiwa na mwalimu kushirikisha wanafunzi katika majadiliano vikundini.Wasailiwa wanafunzi

waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu shughuli zilizofanywa katika majidiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza na maelezo yao yakanakiliwa katika jedwali 4.8.

**Jedwali 4.8: Maelezo ya wanafunzi kuhusu shughuli zifanywazo katika majadiliano vikundini**

| Shughuli za vikundini | Idadi sailiwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Kujadiliana mada | 310 | 64.6 |
| Kusoma | 82 | 17.1 |
| Kuzungumza | 46 | 9.6 |
| Ukariri | 32 | 6.7 |
| Kuimba | 10 | 2.1 |
| Jumla | 480 | 100 |

Kuligana na jedwali 4.8, asilimia 64.6% ya wanafunzi walikubali kwamba shughuli za kufundisha stadi katika vikundi ni majadiliano, asilimia 17.1% ya wanafunzi walikubali kwamba shughuli za kufundisha stadi katika vikundi ni kusoma, hali asilimia 9.6% walikubali kwamba shughuli za kufundisha stadi katika vikundi ni kuzugumza, asilimia 6.7% ni ukariri, hali asilimia 2.1% ya wanafunzi walikubali kwamba shughuli za kufundisha stadi katika vikundi ni uimbaji.

Baadhi ya maelezo ya wanafunzi yanakubaliana na maoni ya Brumfit, Moon na Tongue (1991) waaliodokeza kuwa wanafunzi katika vikundi vya majadiliano wanaweza kujadiliana kuhusu wahusika katika fasihi maoni ambayo yaliungwa mkono na Ndalu (1997) ambaye anasema kuwa shughuli za kufundisha stadi ya kuzungumza vikundini ni kama; uimbaji, ukariri wa mashairi na kutoa maoni.

**Jedwali 4.9: Maelezo ya walimu kuhusu Shughuli zifanywazo katika majadiliano vikundini**

| Shughuli zilizohusishwa | Idadi | Asilimia ( %) |
|---|---|---|
| Ukariri | 1 | 8.3 |
| Kuimba | 1 | 8.3 |
| Kuzungumza | 1 | 8.3 |
| Kusoma | 2 | 16.7 |
| Kujadiliana mada | 7 | 58.3 |
| Jumla | 12 | 100 |

Kulingana na Jedwali 4.9, asilimia 58.3% ya walimu walikubali kuwa shughuli zinahusishwa katika majadiliano ni kujadiliana asilimia 16.7% ya walimu walikubali kwamba shughuli zinahusishwa katika majadiliano ni kusoma , asilimia 8.3% ya walimu walikubali kwamba shughuli zinahusishwa katika majadiliano ni kuzungumza miongoni mwa wanafunzi, asilimia 8.3% ya waalimu ilikubali kwamba shughuli zinahusishwa katika majadiliano ni ukariri na asilimia 8.3% walkubali uimbaji kuhusishwa katika majadiliano vikundini.

Maoni haya yanakubaliana na ya Ndalu (1997) kuwa shughuli muhimu katika majadiliano vikundini kukariri mashairi na dayolojia kwa kutoa maoni miongoni mwa wanafunzi. Walimu wanahimizwa kubuni shughuli mahususi katika majadiliano ya vikundi ili kuimarisha stadi ya kuzungumza kwa ufasaha miongoni mwa wanafunzi kama vile; ukariri wa mashairi, kujadiliana, kuimba nyimbo na mazungumzo.

Hakika matokeo ya utafiti yalidhirisha wazi kuwa kuna uhusiano chanya baina ya majadiliano ya vikundi na stadi ya kuzungumza kwa kuimarika kwa matokeo ya wastani na kipimo cha uwiano cha spearman r=0.75 kwa wanafunzi waliohusishwa katika majadiliano vikundi.

### 4.5 Majukumu katika majadiliano katika Vikundi

Walengwa katika utafiti huu walikuwa na majukumu tofauti katika shughuli za majadiliano vikundini. Wanafunzi wasailiwa waliulizwa wajibu na maelezoyao yakanakiliwa katika jedwali 4.10.

**Jedwali 4.10 Maelezo ya wanafunzi kuhusu wajibu wao katika majadiliano vikundini.**


| Wajibu | Idadi sailiwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Kuongoza | 18 | 3.8 |
| Kuandika | 302 | 62.9 |
| Kusoma | 57 | 11.9 |
| Kujadili | 94 | 19.6 |
| Kuchora | 9 | 1.9 |
| Jumla | 480 | 100 |

Matokeo ya utafiti yadhihirisha kuwa, asilimia 62.9% ya wanafunzi walikubali kwamba wajibu wao katika majadiliano ya vikundi ni kuandika, asilimia 19.6% ya wanafunzi walikubali kwamba wajibu wao katika majadiliano katika vikundi ni kujadili, asilimia 11.9% walikubali kwamba wajibu wao ni kusoma, asilimia 3.8% walikubali kwamba wajibu wao katika majadiliano ya vikundi ni kuongoza na asilimia 1.9% ya wanafunzi walikubali kwamba wajibu wao katika majadiliano ni kuchora.

Maoni yaliyotolewa na wanafunzi yanasabihiana na ya Clark (1971) kuwa vikundi vya kujadiliana vinafaa kuongozwa na wanafunzi wenyewe. Mwalimu anafaa kuwa mwelekezi na mwandalizi wa mazingira bora ya kujadiliana na kushiriki katika uundaji wa vikundi vya majadiliano.

Lembo (1972) pia aliakisi maelezo ya wanafunzi kuwa mbali na uongozi wa kikundi, wanafunzi wana jukumu la kutoa maoni na kushiriki kikamilifu katika shughuli za vikundini. Hata hivyo asilimia kubwa ya wanafunzi 62.9% walikinzana wazo hili waliposema kuwa jukumu lao ni kuandika. Hii yadhihirisha kuwa wanafunzi wengi wanaoshiriki katika majadiliano ya vikundi huchukua muda mrefu kunakili yajadiliwayo vikundini badala ya kumakinika na kushiriki ipasavyo katika shughuli za vikundini. Bila shaka hali hii huweza kuchangia kutokuza uwezo kutoa maoni basi kulemaza stadi ya kuzungumza.

Walimu wahimizwa kuhakikisha kuwa wanashirikisha wanafunzi wote katika utoaji wa maoni vikundini ili kukuza stadi ya kuzungumza kwa ufasaha na kwa mantiki katika stadi ya kuzungumza. Katika kufanikisha shughuli vikundini, walimu wanafaa kuelewa wajibu wao.Walimu wateuliwa waliulizwa kuhusu wajibu wao katika majadiliano ya vikundi na maoni yao yakanakiliwa katika mchoro 4.




**Mchoro 4: Chati inayoonyesha wajibu wa waalimu katika majadiliano vikundini**

Matokeo ya utafiti na yalidhihirisha kuwa, asilimia 83.3% ya walimu walikubali kwamba wajibu wao katika majadiliano ni kuelekeza na asilimia 16.7% wakakubali


kuwa wajibu wao katika majadiliano vikundini ni kuongoza.Inadhihirika kuwa walimu wengi wanatambua kuwa wajibu wao katika majadiliano vikundini ni kuelekeza wanafunzi wala si kuongoza. Maoni haya ni sawa na ya Lembo (1972) kwamba mwalimu ni mwelekezi anayeandaa mazingira ya kujifunza katika majadiliano vikundini na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika majadiliano. Wajibu wa walimu ni muhimu majadiliano ya vikundi. Kuwepo kwa walimu katika vikundi vya majadiliano huwapa wanafunzi motisha na mwelekeo wanaposhiriki katika shughuli za vikundini na kuepusha changamoto zinaweza kuibuka wanafunzi wakiwa peke yao. Maoni ya Clark (1971) pia yaliwiana na matokeo haya kwa kumwona mwalimu kama kiongozi wa kuhusisha wanafunzi katika majadiliano. Hakika mwalimu ni kiongozi tena mfano wa kuigwa na wanafunzi anaowafunza.Bila shaka mwanafunzi mzuri ni zao la maelekezo ya mwalimu. Mwalimu ana wajibu wa kuhimiza wanafunzi wote kushiriki katika majadiliano kwa kutoa maoni hivyo basi kukuza stadi ya kuzungumza.

## 4.6 Manufaa wa Majadiliano ya Vikundi

Sehemu hii iliwasilisha na kujadili maoni ya wanafunzi na walimu kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi kwa mujibu wa hojaji zilizojazwa. Matokeo ya tathmini ya wanafunzi waliohusishwa yakilinganishwa na ya wale wasiohusishwa katika majadiliano ya vikundi.

### 4.6.1 Maelezo ya Wanafunzi kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi

Wanafunzi wengi waliosailiwa katika shule zilizoteuliwa walisema kuwa majadiliano ya vikundi yana manufaa inavyodhihirishwa katika mchoro 5.




**Mchoro 5: Chati inayoonyesha maelezo ya wanafunzi kuhusu manufaa ya Majadiliano ya Vikundi**

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa, asilimia 42.5% ya wanafunzi walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni kuelewa, asilimia 17.9% ya wanafunzi walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni kuelekezana, hali asilimia 16.3% ya wanafunzi walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano Katika vikundi ni kufikirisha, asilimia 14.4% ya wanafunzi walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni kuchangiana na asilimia 9 % ya wanafunzi walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni ushirikiano.

Maelezo haya ni sawa na maoni ya Kokemuller (2007) kwamba majadiliano ya vikundi ni njia moja ya kuleta ushirika miongoni mwa wanafunzi, kufikirisha na kuendeleza uelewaji wa mada. Maoni ya Brown (2007)yanakubaliana na matokeo

haya kwani alidokeza kuwa mbinu ya majadiliano ya vikundi husaidia wanafunzi kuelewa mambo na kuyakumbuka kwa muda mrefu.

Maelezo yao pia ni sawa na Vygotsky (1978) aliyedokeza kuwa majadiliano ya vikundi husaidia wa wanafunzi kushirikiana kutoa maoni na kuwafikirisha. Ni wajibu wa walimu kuelekeza wanafunza vyema na kuwaandalia shughuli ambazo zitaimarisha uewaji wao na kushiriki kwao ili kukuza stadi ya kuzungumza. Maoni sawia na hayo yaliittolewa na Dunne (1990) katika utafiti wake ambapo wanafunzi waliohusishwa katika majadiliano ya vikundi walipata alama bora kuliko wale hawakuwa katika vikundi. Ni wajibu wa mwalimu kuwaelekeza wanafunzi vyema na kuwashirikisha wote katika majadiliano vikundini ili kuimarisha uelewaji wa wa mada , kukuza ushirikiano na kukuza stadi ya kuzungumza na uwezo wa kuwasiliana vyema.

### 4.6.2 Maelezo ya walimu kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi

Majadiliano katika vikundi huandaliwa na kuelekezwa na walimu kama ilivyodokezwa katika majukumu ya walimu katika majadiliano ya vikundi. Kila mwalimu huwa na malengo mahususi wakati wa kutumia majadiliano vikundini pia huwazia manufaa fulani katika shughuli za vikundini.Walimu teuliwa waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi na maoni ya yakanakiliwa katika jedwali 4.11.

**Jedwali 4.11: Maelezo ya walimu kuhusu manufaa ya majadiliano katika vikundi.**

| Manufaa ya majadiliano vikundini | Idadi sailiwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ushirikiano | 43 | 8.3 |
| Kufikrisha | 78 | 16.3 |
| Kuchangiana mawazo | 69 | 14.4 |
| Kuelekezana | 86 | 17.9 |
| Kuelewa mada | 6 | 50 |
| Jumla | 480 | 100 |

Idadi kubwa ya walimu walikubali kuwa manufaa makubwa ya majadilano ya vikundi ni kuelwa mada inayofundishwa na mwalimu mmoja tu alikubali kuwa manufaa makuu ni kuchangiana mawazo ambayo huweza kukuza stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi.

Kulingana na jedwali 4.11, utafiti ulionyesha kuwa asilimia 50% ya walimu walikubali kwamba manufaa ya majadiliano ya vikundi ni kuelewa mada, asilimia 16.7% ya walimu walikubali kwamba manufaa ya majadiliano ya vikundi ni kuelekezana miongoni mwa wanafunzi, asilimia 16.7% ya walimu walikubaliana kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni kufikirisha miongoni mwa wanafunzi, asilimi 8.3% ya walimu walikubali kwamba manufaa ya majadiliano katika vikundi ni kuchangiana mawazo miongoni mwa wanafunzi na asilimia 8.3% ya walimu walikubali kwamba manufaa ya majadiliano ya vikundi ni ushirikiano miongoni mwa wanafunzi.

Kutokana na data hii, ni wazi kuwa walimu wengi hawatumii mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza bali kutaka kuhakikisha wanafunza

wameelewa mada inayafunzwa. Ni dhahiri kuwa wanafunzi wanaponyimwa nafasi ya kuongea vikundini na kutegemea tu kuandika hoja za kuwaelewesha mada, huenda wasikuze uwezo wa kuongea.

Matokeo utafiti yanalingana na maoni ya Gathumbi na Masembe (2005) kuwa wanafunzi wengi huwa na matatizo ya kuzungumza kwa ufasaha kwa vile wanakosa kushirikishwa katika stadi ya kusikiliza na kuongea. Walipendekeza kuwa stadi hizi mbili zafaa kuzingatiwa wakati wa kufundisha lugha. Maoni sawia na haya pia yalitolewa na Kimemia (2001) ambaye alikosoa mfumo ambapo walimu hufanya wanafunzi kubugia wanayofundishwa bila kupewa nafasi kushiriki katika kutoa maoni yao.Walimu wanahimizwa kutilia mkazo matumizi ya majadiliano katika vikundi sio tu kufundisha wanafunzi kuelewa mada bali pia kufundishia stadi ya kuzungumza.

### 4.6.3 Uchanganuzi wa matokeo ya mtihani wa kwanza na wa mwisho

Mtihani wa kwanza na mwisho ulipewa wanafunzi wa kidato cha pili katika shule sita zilizoteuliwa. Mtihani wa pili ulifanywa baada ya miezi miwili baada ya wanafunzi kushirikishwa katika majadiliano ya vikundi. Wanafunzi 229 walihusishwa ili kutathmini umilisi wao wa stadi ya kuzungumza kabla na baada ya matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi. Matokeo yao ya alama wastani yaliwasilishwa katika jedwali 4.12.

**Jedwali 4.12: Matokeo linganishi ya mtihani wa kwanza na mwisho kuchunguza manufaa ya majadiliano ya vikundi kufunzia stadi ya kuzungumza.**

| Shule | Kundi | Idadi | Alama Wastani (%) Mtihani Wa Kwanza | Alama Wastani (%) Mtihani Wa Pili | Alama Wastani (%) Mitihani Miwili |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Husishwa | 22 | 60 | 82 | 71 |
| | Lisilohusishwa | 21 | 64 | 66 | 65 |
| B | Husishwa | 15 | 56 | 70 | 63 |
| | Lisilohusishwa | 16 | 60 | 62 | 61 |
| C | Husishwa | 21 | 70 | 84 | 72 |
| | Lisilohusishwa | 20 | 66 | 66 | 66 |
| D | Husishwa | 15 | 68 | 80 | 74 |
| | Lisilohusishwa | 14 | 58 | 60 | 59 |
| E | Husishwa | 19 | 56 | 72 | 64 |
| | Lisilohusishwa | 18 | 60 | 60 | 60 |
| F | Husishwa | 23 | 66 | 76 | 71 |
| | Lisilohusishwa | 24 | 64 | 64 | 64 |

Kutokana na jedwali 4.1, makundi ya wanafunzi yaliyohusishwa katika majadiliano ya vikundi yalionyesha kuimarika kwa matokeo yao kwa alama wastani. Matokeo ya shule A yaliimarika kwa alama wastani 60 % hadi 82%, shule B alama 56% hadi 63%, shule C alama 70% hadi 84%, shule D alama 68% hadi 80%, shule E alama 56% hadi 72%, shule F alama 66% hadi 76%. Hata hivyo matokeo ya alama wastani za makundi ambayo hayakuhusishwa katika majadiliano ya vikundi hayakuimarika sana. Kwa mfano alama wastani ya shule A yaliimarika kidogo sana kutoka alama wastani 60% hadi 62%, shule C kubaki alama 66% katika mitihani yote miwili, shule

D alama 58% hadi 60%, shule E alama wastani 60% katika mtihani wa kwanza na wa pili na shule F alama wastani 64% katika mitihani yote miwili. Kwa kuzingatia alama za kundi husishwa na lisilohusishwa umbali baina ya makundi hayo ni mkubwa baada ya matumizi ya majadiliano ya vikundi mfano shule A umbali ni alama 04 kabla na alama 16 baada ya matumizi ya majadiliano ya vikundi kudhihirisha kuwa majadiliano ya vikundi yaliimarisha stadi ya kuzungumza miongoni wanafunzi waliohusishwa.

Matokeo ya baadhi ya vikundi visivyohusishwa katika majadiliano vikundini yaweza kuimarika kidogo. Hili liliweza kutokea pengine kwa sababu ya vigeu viingilizi kama sera ya shule kuhusu matumizi ya lugha, mielekeo ya wanafunzi na kutagusana kwa wanafunzi wa makundi hayo mawili. Hii inaonyesha kuwa kutangamana kwa wanafunzi huweza kuchangia kuimarika kwa stadi ya kuzungumza kwa kiasi fulani. Kutokana na matokeo ya mtihani tangulizi na wa mwisho, majadiliano ya vikundi yaliimarisha stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi waliohusishwa kinyume na makundi ya wanafunzi ambayo hayakuhusishwa katika majadiliaono ya vikundi.

Mitihani hiyo ililenga kuchunguza uhusiano kati ya matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi na umilisi wa stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili katika Tarafa ya Mosocho.

Matokeo haya ni dhihirisho kuwa majadiliano ya vikundi yana manufaa ya kukuza stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi. Matokeo haya yanakubaliana na maoni ya Kokemuller (2007), Geoffrey (1993) na Brown (2007) kuwa majadiliano ya vikundi hukuza stadi ya kuwasiliana vyema miongoni mwa wanafunzi. Kwa kweli

lengo kuu la kufunza lugha ni kukuza uwezo wa kuzungumza na kuwasiana kwa ukakamavu na ufasaha. Walimu hawana budi kushirikisha wanafunzi katika vikundi kwa kusudi la kuimarisha stadi ya kuzungumza kwa ukakamavu na ufasaha.

Kuhusu shughuli zinazofanywa katika vikundi, maelezo yaliyotolewa na idadi wanafunzi kubwa ya wanafunzi (66%) yalidhihirisha kuwa shughuli waifanyayo katika majadiliano vikundini ni kujadiliana mada walizopewa kushughulikia. Wanafunzi wachache (9.8%) walisema kuwa shughuli kuu vikundini ni kuzungumza. Dhihirisho ni kwamba mbali na kulenga mada inayojadiliwa walimu hawahimizi wanafunzi kuzungumza ili kukuza stadi ya kuzungumza. Hili lilithibitishwa pia katika maelezo ya wanafunzi kuhusu manufaa ya majadiliano ya vikundi ambapo wanafunzi 204 walisema kuwa manufaa ya majadiliano ya vikundi ni kuelewa mada ijadiliwayo.Wanafunzi 69 walisema kuwa manufaa ya majadiliano ni kuchangiana mawazo kwa kutoa maoni vikundini. Licha ya hayo, idadi kubwa ya wanafunzi 302 walisema kuwa jukumu lao kubwa katika majadiliano vikundini ni kuandika, kuonyesha kuwa wengi wao hunakili maoni ya wengine bila wao wenyewe kushiriki kutoa yao. Hali hii haisaidii mwanafunzi kukuza uwezo wa kuwasiliana kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili hata wakimudu kupita mtihani kidato cha nne vyema.

Maelezo ya wanafunzi yanaoana na maoni ya Babusa(2010) kuwa walimu wengi hufunza kwa minajili ya mitihani ya kitaifa wala si kukuza stadi zote za lugha.Walimu hushughulikia stadi andishi kwa vile ndizo hutahiniwa na kupuuza stadi zungumzi ambazo hazitahiniwi.Wanafunzi hatimaye hupata alama nzuri katika mtihani lakini hushindwa kuwasiliana kwa ufasaha katika lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya yalionyesha kuwa pengine walimu hawaelekezi wanafunzi vyema kuhusu wajibu wao katika majadliano ya vikundi. Ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wote hushiriki katika kutoa maoni wakiwa vikundini pia kuhimiza wanafunzi wanyamavu kuzungumza. Hili likifanyika wanafunzi watanufaika si tu katika kuelewa mada ijadiliwayo bali pia kukuza uwezo wa kuwasiliana vyema na kwa ufasaha .

Majadiliano katika vikundi yakiandaliwa vyema wanafunzi huweza kuimarisha uwezo wao wa kuzungumza kwa ufasaha. Kwa kurejelea ulinganisho wa alama za mtihani tangulizi na wa mwisho kulidhihirika kuimarika kwa alama za wanafunzi husishwa ikilinganishwa na wanafunzi ambao hawakushirikishwa katika majadiliano vikundini. Hili ni dhihirisho la kuwa uhusiano chanya kati ya mbinu ya majadiliano ya vikundi na ukuzaji wa stadi ya kuzungumza.

### 4.7 Changamoto zikumbazo Majadiliano ya Vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza

Wanafunzi waliosailiwa waliulizwa baadhi ya Changamoto zilizokumba majadiliano ya vikundi na maoni yao yakanakiliwa katika jedwali 4.13.

**Jedwali 4.13: Maelezo ya wanafunzi kuhusu changamoto katika majadiliano vikundini**

| Changamoto | Idadi | Asilimia ( %) |
|---|---|---|
| Uzembe | 288 | 60 |
| Kuchelewa | 71 | 14.8 |
| Kutegemeana | 54 | 11.3 |
| Kuzozana | 39 | 8.1 |
| Kutofanya utafiti | 28 | 5.8 |
| Jumla | 480 | 100 |

Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba asilimia 60% ya wanafunzi walikubali kwamba changamoto zikumbazo majailiano vikundini ni kutofanya utafiti, asilimia 14.8% uzembe, asilimia 11.3%, asilimia 8.1% kuchelewa na asilimia 5.8% yao walikubali kwamba changamoto zikumbazo majadiliano katika vikundi ni kuzozana.

Maelezo ya baadhi ya wanafunzi yamedhihirishwa na Dunne na Bennett (1990) kuwa changamoto kubwa katika majadiliani vikundini miongoni mwa wanafunzi ni uzembe, kuzozana na kutofanya shughuli waliyopewa. Ni jukumu la mwalimu kuelekeza wanafunzi vyema vikundini ili kuepukana na changamoto ziwezazo kuibuka miongoni mwa wanafunzi wakati wa majadiliano ya vikundi. Walimu wahakikishe kuna vifaa vya kutosha vikundini, wachanganye wanafunzi vyema, watie wanafunzi motisha wakiendelea na shughuli vikundini na kughulikia changamoto zozote zitokeapo vikundini.

Walimu waliohusishwa katika utafiti waliuliza kutoa maelezo kuhusu changamoto zilizokumba matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza. Maelezo yao yalinakiliwa katika jedwali 4.14.

**Jedwali 4.14: Maelezo ya walimu kuhusu changamoto za majadiliano vikundini.**

| Changamoto | Idadi | Asilimia( %) |
|---|---|---|
| Kutofanya utafiti | 7 | 66.7 |
| Kuchelewa | 2 | 16.7 |
| Kutegemeana | 1 | 8.3 |
| Kuzozana | 1 | 8.3 |
| Uzembe | 1 | 8.3 |
| Jumla | 12 | 100 |

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa, asilimia 66.7% ya walimu walikubali kwamba changamoto zinazokumba majadiliano katika vikundi ni kutofanya utafiti miongoni mwa wanafunzi, asilimia 58.3% ya walimu walikubali kwamba changamoto zinazokumba majadiliano katika vikundi ni uzembe miongoni mwa wanafunzi, asilimia 8.3% ya walimu walikubali kwamba changamoto zinazokuba majadiliano katika vikundi ni kuchelewa miongoni mwa wanafunzi, asilimia 8.3% ya walimu walikubali kwamba changamoto zinazokumba majadiliano katika vikundi ni kutegemeana miongoni mwa wanafunzi na asilimia 8.3% ya walimu ilikubali kwamba changamoto zinazokumba majadiliano katika vikundi ni kuzozana miongoni mwa wanafunzi kwa vile kila mmoja hutaka kupata nafasi kutoa maoni.

Asilimia kubwa ya walimu walisema kuwa kufanya utafiti ni changamoto kuu kwa wanafunzi katika majadiliano ya vikundi. Ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wana muda kufanya utafiti kuhusu mada wanayoshughulikia pia kuwe na utaratibu wa kila mwanafunzi kutoa maoni ili kukuza stadi ya kuzungumza.

Maelezo ya wasailiwa wengi yaliwiana na maoni ya Ohair naWiemann (2004) kuwa wanafunzi wengi hawapati nafasi kushiriki katika kutoa maoni kwa vile kila mmoja katika kikundi hutaka kuongea. Matokeo ya utafiti pia yaliwiana na ya Dunne na

Bennet (1992) kuwa uzembe miongoni mwa wanafunzi na wanafunzi kutofanya shughuli vikundini au kukataa kutoa mchango vikundini ni changamoto kuu katika majadiliano ya vikundi. Walimu wanahimizwa kubuni mikakati ya kuepusha changamoto zinazoweza kuathiri majadiliano ya vikundi na kuhakikisha ushiriki wa wanafunzi wote sio katika kusikiliza na kuandika hoja bali pia kutoa maoni (kuzungumza).

Data ilichanganuliwa kupitia kipimo cha uwiano r=0.75, ilidhihirisha kuwa mabadiliko katika kigeu huru yalisababisha mabadiliko katika kigeu tegemezi. Hivi ni kuonyesha kuwa na uhusiono chanya kati ya vigeu hivi. Vilevile kipimo cha mtawanyiko wa alama na cha wastani vilionyesha uhusiano wa mkubwa sana kati ya matumizi ya majadiliano ya vikundi na stadi ya kuzungumza. Walimu kama waelekezi wana jukumu la kushirikisha wanafunzi kikamilifu katika majadiliano ya vikundi ili kukuza stadi ya kuzungumza.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO YA MADHUMUNI YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni muhimu kwa vile inatoa muhtasari wa utafiti, hitimisho, mapendekezo na maelekezo kuhusu utafiti wa baadaye. Mapendekezo yalitolewa huweza kutegemewa na washika dau katika sekta ya elimu kubuni sera na mikakati ya kuimarisha ufundishaji wa stadi ya kuzungumza. Maelezo katika sura hii husaidia msomaji kuelewa ufaafu wa matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika shule za upili tarafa ya Mosocho,Kaunti ya Kisii, Kenya.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Kutoka na utafiti huu, ilithibitishwa kuwa asilimia 87.5% ya wanafunzi wana vikundi vya majadiliano katika shule zao. Hii asilimia imeunda vikundi vya majadiliano shuleni mwao. Asilimia 12.5% ya wanafunzi walikanusha kwamba hawana vikundi vya majadiliano shuleni mwao. Inaamanisha walimu hawawahusishi wanafunzi katika majadaliano pengine kwa kutoelewa manufaa yake . Ilitibishwa pia kuwa asilimia 75% ya waalimu walikuwa na vikundi vya majadiliano katika shule zao na hali asilimia 25% ya walimu hawakuwa na vikundi vya majadiliano katika shule zao. Hata kama idadi isiyoshirikishi katika majadiliano ya vikundi ni ndogo, inadhihirisha wazi kuwa baadhi ya walimu hawaelewi umuhimu wake. Huenda walimu hukosa kuitumia kwa sababu mielekeo hasi kuhusu majadiliano ya vikundi.

Katika kutambua shughuli zilizofanywa na wanafunzi vikundini**,** ilithibitishwa kuwa asilimia 66% ya wanafunzi walitambua shughuli zinazofanywa katika kujadiliana

mada, asilimia 17.1% kusoma, asilimia 10% kuzungumza, asilimia 6.5% kukariri na asilimia 2.1% ya wanafunzi ilikubali kuwa shughuli zinazofanyika wakati wa majadiliano ni kuimba. Wanafunzi wafaa kuelekezwa kuwa kujadili mada si shughuli muhimu zaidi katika majadiliano ya vikundi bali kukuza uwezo wa kuwasiliana vyema na wenzao.

Kupitia maelezo ya walimu, ilithibitishwa kuwa asilimia 58.3% ya walikubali kuwa shughuli inayotumika zaidi katika majadiliano ni kujadiliana, asilimia 16.7% kusoma, asilimia 8.3% kukariri, asilimia 8.3% ya waalimu walikubali kwamba shughuli inayotumika katika majadiliano ni kuzungumza. Walimu wengi hutumia majadiliano kufunzia mada watakazo wanafunzi kuelewa si kukuza uwezo wa kuwasiliana.

Katika kutambua majukumu ya mwalimu na mwanafunzi katika majadiliano katika vikundi kufundisha stadi za kuzungumza, ilithibitishwa kuwa majukumu ya asilimia 83.3% ya walimu ilikuwa kuwaelekeza wanafunzi, asilimia 16.7% ya walimu ilikuwa kuongoza wanafunzi. Ilitibishwa kuwa asilimia 62.9% ya wanafunzi walisema majukumu yao ni kuandika, asilimia 19.6% kujadili, asilimia 11.9% kusoma, asilimia 3.8% kuongoza na asilimia 1.9% ya wanafunzi kuchora. Ni wazi kuwa jukumu kuu la wanafunzi ni kuandika. Walimu wafaa kuwaeleza wanafunzi katika kujadiliani au kutoa maoni yao vikundini ili kukuza stadi ya kuzungumza.

Kuhusiana na manufaa ya majadiliaono ya vikundi, asilimia 42.5 % ya wanafunzi walikubaliana kuwa manufaa ya makuu ni kuelewa mada, 17.9% kuelekezana, 16.3 kufikirisha, 14.4%, kuchangiana mawazo na 8.9% ushirikiano. Utafiti ulibainisha kuwa kuchangiana mawazo au kuzungumza ndiyo manufaa makuu ikizingatiwa kuwa

ndicho kigezo kikuu cha kuboresha stadi ya kuzungumza kama ilivyodhihika kwa kipimo cha wastani

Katika kuchunguza changamoto zinaweza kukumba mbinu ya majadiliano katika vikundi wakati wa kufundisha stadi ya kuzungumza,ilithibitishwa kuwa asilimia 60% ya wanafunzi walisema changamoto kuu ni kutofanya utafiti, asilimia 14.7% uzembe, asilimia 11.3% ya kutegemeana, asilimia 8.1% ya kuchelewa na asilimia 5.8% ya wanafunzi ni kuzozana. Ilitibishwa kuwa asilimia 66.7% ya walimu walisema changamoto kuu ni kutofanya utafiti miongoni mwa wanafunzi, asilimia 16.7% uzembe miongoni mwa wanafunzi, asilimia 8.3% kuchelewa kumaliza shughuli, asilimia 8.3% kutegemeana , changamoto ya asilimia 8.3% kuzozana miongoni mwa wanafunzi.

Maelezo ya asilimia kubwa ya walimu na wanafunzi yaonyesha kuwa changamoto kuu ni kutofanya utafiti. Walimu wafaa kutenga muda wa kutosha kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusu mada kabla ya kujadiliana. Hii itawafanya kutoa maoni vikundini hivyo kuimarisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa ukakamavu na ufasaha.

**5.3 Hitimisho**

Kutokana na utafiti, imebainishwa kwamba mbinu ya majadiano ya vikundi huweza kukuza stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili. Walimu huwa na vikundi vya majadiliano shuleni ingawa baadhi yao hawaewi manufaa mengi ya kuitumia kufundisha stadi ya kuzungumza mbali na kutumiwa katika kufundishia mada mbalimbali. Ilibainishwa katika utafiti kuwa walimu wengi hushughulikia stadi andishi kwa vile ndizo hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa.Hali

hii hufanya wanafunzi kukosa umilisi wa stadi ya kuzungumza hata kama wamefanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Ukosefu wa muda wa kufanya utafiti kwa wanafunzi ni changamoto kuu ambayo inakumba wanafunzi na walimu wakati wa majadiliano ya vikundi. Hali hii itokeapo wanafunzi hukosa huwezo kuchangiana mawazo na kukosa uwezo wa kuwasiliana na hivyo kukosa kukuza stadi ya kuzungumza.

Katika uundaji wa vikundi vya majadiliano walimu huzingatia uwezo wa wanafunzi kimasomo na kikundi hakipasi kuwa na wanafunzi zaidi ya watano.Wanafunzi zaidi ya watano hukosa mshikamano hivyo kuzua vujo katika vikundi. Kila kikundi kiwe na malengo mahususi ya kuafikiwa kufikia mwisho wa majadiano ya vikundi.

Ukariri na uimbaji haukutiliwa mkazo kama mojawapo ya shughuli za majadiliano vikundini. Kutokana na matokeo ya utafiti, walimu na wanafunzi huzingatia zaidi kujadili mada kama shughuli kuu vikundini. Hii huchangia wanafunzi kutokuza stadi ya kuzungumza kwa vile wengi wao hulenga kuelewa mada ili kufanya vyema katika mitihani. Majukumu ya walimu ya kuwaelekeza wanafunzi katika majadiliano nao wanafunzi huwa na jukumu la kuongoza vikundi na kushiriki katika kutoa maoni. Hii huchangia mno katika uthabiti wa vikundi vya majadiliano na hatimaye husaidia katika kukuza stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

## 5.4 Mapendekezo

Miongoni mwa malengo ya ruwaza ya mwaka 2030 ni kuhakikisha mafundisho bora ili kuwapa wanafunzi ujuzi wa hali ya juu. Mafundisho haya yanashirikisha

ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano. Malengo ya ufundishaji lugha ya Kiswahili katika shule za upili yaweza kuafikiwa ikiwa stadi zote za lugha zitahusishwa wakati wa kufundisha. Kusikiliza na kuongea ndizo stadi za kwanza katika mtaala wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulibainisha kuwa si walimu wote hutumia majadiliano ya vikundi katika kufundisha stadi ya kuzungumza. Inapendekezwa kuwa walimu wakuu wakishirikiana na wizara ya elimu waandae semina zitakazoongozwa na wataalamu wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kuhamasisha walimu kuhusu matumizi ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza.

Utafiti ulidhihirisha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya majadiliano ya vikundi na umilisi wa stadi ya kuzungumza. Inapendekezwa kuwa walimu wote wahimize wanafunzi kutilia maanani majadiliano ya vikundi kwa kuwa huweza kuimarisha stadi ya kuzungumza.

Baadhi ya walimu walidhani jukumu lao ni kuongoza wanafunzi. Pendekezo ni kwa walimu kuelewa majukumu yao na kufunzdisha wanafunzi namna ya kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya vikundi kwa vile wengi wanaamini jukumu lao kuu ni kuandika.Wanafunzi wanafaa kushirikishwa katika vikundi, wajiongoze wenyewe na kuhakikisha kuwa wote wanatoa maoni yao ili kuondoa tatizo la wanafunzi wengi kukosa umilisi wa lugha ya Kiswahili.

Ni yakini kwamba walimu wengi waliosailiwa hawakuhusisha shughuli nyingi ambazo zinaweza kuimarisha stadi ya kuzungumza miongoni mwa wanafunzi pia

walitegemea zaidi kujadiliana kama shughuli kuu. Pendekezo ni kwamba walimu wahusishe mbinu zaidi kama vile maigizo ya vipera vya fasihi mfano tamthilia, hadithi fupi na malumbano ya utani, miviga, soga, mawaidha na ulumbi kufundishia stadi ya kuzungumza katika shule za upili.

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa kuna changamoto nyingi zinazokumba majadiliano ya vikundi miongoni mwa wanafunzi katika kufundishia stadi ya kuzungumza. Pendekezo langu ni kwamba walimu wakuu kupitia wizara ya elimu wahakikishe kuwa kuna vifaa vya kutosha shuleni kama vile; vitabu vya kuongoza wanafunzi kufanya utafiti wanapokuwa na majadiliano ya vikundi pia wanafunzi wahamasishwe kufanya utafiti wa kina kabla ya kuhusika katika maoni wakati wa majadiliano vikundini na mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wazembe na wakimya wanashiriki kikamilifu katika majadiliano vikundini ili kukuza stadi ya kuzungumza. Inapendekezwa pia kuwa utafiti zaidi unafaa kufanywa kuhusu mbinu nyingine ambazo zinawezakutumiwa kuimarisha stadi ya kuzungumza.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti wa baadaye

Utafiti wa baadaye unahitaji kuangazia sehemu zifuatazo:-

a) Kwa vile utafiti huu ulihusu matumizi ya majadiliano ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, inapendekezwa kuwa utafiti kama huu ufanywe katika tarafa nyingine za Kaunti ya Kisii.

b) Kwa vile utafiti ulishughulikia stadi ya kuzungumza utafiti zaidi unafaa kufanyiwa stadi nyingine za lugha.

**MAREJELEO**


Bachman, L.F. (1990). Fundamental Consideration in Language Testing. Oxford. Oxford University Press.

Barbara, G.D. (1993). Collaborative Learning: Group Work and Study teams. San Francisco. Jossey-Bass Publishers.

Bennet, N. & Dunne, B. (1992). Managing classroom groups. Cheltenham: Stanley Thorne.

Brown, H.D. (2007). Teaching by principles: An intergrative approach to language pedagogy. (Third Edition) White Plains NY:Pearson Longman.

Brumfit, C. (1991). Teaching English to children: From practice to principle. London.Harper Collins publishers.

Clark, D.H. (1971). Humanistic Teaching. Ohio. Charles merril publishing company.

Creemers, B.P. (1994). Effective classroom. London: Cassel.

Dunne, E. & Bennet, N. (1990). Talking and learning in groups. London: Macmillan education Ltd.

Galanes, G & Adams, K. (2013). Effective group discussion: Theory and practice. Newyork.MCGraw.Hill

Gathumbi, A. W. & Masembe, S.(2005). Principles & Techniques in Language teaching. Nairobi: JKF.

Geoffrey, P. (1993). Teaching today: Apractical guide. London: Stanley Nelson Thorne publishers.

Ingule, F. & Gatumu, H. (1996). Esssentials of Educational Statistics. Nairobi. East African Educational Publishers.

Kagan, S. (1988). Co-perative learning ,Resources for teachers. Califonia: University of califonia. .

Kimemia, J. (2001). Kiswahili: The dilemma of developing the national language. Njoro Egerton University press.

Kokemuller, N. (2007). Effective Group Discussion: Theory and Practice. Newyork. McGrow-Hill.

Kombo, D. & Tromp, D. (2006). Project and thesis writing: An introduction. Nairobi: Pauline publishers Africa.

Kothari,C.R. (2011). Research methodology: Methods and Techniques. 2nd Edition.Books google.Com.

Lembo, J.M. (1972). Learning and teaching in todays schools. Ohio: Bell and Howel Company.

Malamah, T. (1987). Classroom interaction. Oxford: Oxford university press.

Mligo, E.S. (2012). Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye mantiki. Dar es Salaam. EcumenicalGathering (EGYS).

Mugenda , O. & Mugenda, A. (2003). Research methods: Quantitative and qualitative approaches. (Revised edition). Nairobi: Act press.

Muthuuri, D.G. (2000). Code Switching among Kenyatta University multilingual community: Unpublished MA Thesis. Nairobi. Kenyatta University.

Mwei, K.P.(2010). Independent Study in Research and Theory and Curriculum. Unpublished PhD Paper. Eldoret. Moi University.

Ndalu, A. (1997). Mwangaza wa Kiswahili. Nairobi:East African Educational Publishers.

O'hair, D. & Wiemann, M. (2004). The Essential guide to group communication. Boston. Bedford.

Orodho, A.J & Kombo, D, K. (2002). Research Methods.Nairobi.Kenyatta University Institute of open Learning.

Orodho, J.A. (2004).Techniques of writing research proposal and report in education and social sciences. Nairobi: Masola publishers.

__________(2005). Elements of educational and social science research methods. Nairobi: Masola Publishers.

Owen, R. (1998). Organisational Behavior in Education. London: Allyn & Bacon, PrenticeHall inc.

Richards, J. & Rodgers. (2001). Approaches and Methods in Language Teaching. Cambridge. Cambridge UniversityPress.

Vigotsky, C. (1978). Mind in Society. Cambridge. Havard University Press.

Wamitila, K.W. (2003). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na andishi.Nairobi. Focus Publications.

Wiersman , O .Z. (1985). Research methods in education:An introduction. London: Allyn & Bacon.

Yuko,W.O. & Orien.D. (2005).Writing Research Proposal and Report. Kisumu. Options Printers and Publishers

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO I: HOJAJI KWA WANAFUNZI

Utafiti huu ulinuiwa kwa madhumuni ya kielimu tu. Ulilenga matumizi ya mbinu ya majadiliaono ya vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Hojaji hii imegagwanywa katika sehemu mbili kuu. Tafadhali jibu maswali yote kwa uaminifu naufasaha. Mtafiti anakujuza kuwa habari utakayotoa itawekwa siri na kutumiwa kwa utafiti huu tu.

Tia alama sahihi(√ ) panapofaa ama jaza habari inayohitajika katika nafasi zilizoachwa**.**

**SEHEMU YA A. Habari /maelezo ya kibinafsi.**

Sehemu hii inadhamiria kutafuta habari/ maelezo kukuhusu na shule yako.Tafadhali tia alama sahihi (√) panapofaa katika mabano ama jaza maelezo panapohitajika.

1. Jinsia Mume ( ) Mke ( )
2. Kidato chako Kwanza ( ) Pili ( ) Tatu ( ) Nne ( )
3. Aina ya shule Kutwa ( ) Bweni ( )

**SEHEMU YA B**

Sehemu hii inadhamiria kukusanya habari kuhusu swala linalotafitiwa. Tia alama ( ) panapofaa.

1. Je, kuna matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi darasani?

   Ndio ( ) La ( )

2. Ni shughuli gani zinahusishwa katika kufundishia stadi ya kuzungumza vikundini ? Ukariri ( ) Uimbaji ( ) Kuzungumza ( ) Kusoma ( )

   Kujadili ( ) Majadiliano ( )

3. Wajibu wako ni upi katika majadiliano vikundini ?

   Kuongoza ( ) Kuandika ( ) Kusoma ( ) Kujadili ( ) Kuchora ( )

4. Kwa maoni yako majadiliano katika vikundi yana manufaa gani?

   Ushirikiano ( ) Kufikirisha ( ) Kuchangiana mawazo ( ) Kuelekezana ( ) Kuelewa somo ( )

5. Ni changamoto zipi zinakumba majadiliano katika vikundi?

   Uzembe ( ) Kuchelewa ( ) Kutegemeana ( ) Kuzozana ( ) Kutofanya utafiti ( )

**SHUKRANI KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO II: HOJAJI KWA WALIMU

Utafiti huu unadhamiriwa kwa madhumuni ya kielimu tu.Utalenga matumizi ya mbinu ya majadiliano katika vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Hojaji hii imegawanywa katika sehemu mbili kuu. Tafadhali jibu maswali yote kwa uaminifu na ufasaha. Mtafiti anakujuza kuwa habari utakayotoa itawekwa siri na kutumiwa kwa utafiti huu tu. Tia alama sahihi (√) panapofaa ama jaza habari inayohitajika katika nafasi zilizoachwa.

**SEHEMU YA A. Habari /maelezo ya kibinafsi.**

Sehemu hii inadhamiria kutafuta habari/ maelezo kukuhusu na shule yako.Tafadhali tia alama sahihi (√) panapofaa katika mabano ama jaza maelezo panapohitajika.

1. Jinsia Mume ( ) Mke ( )
2. Kiwango cha Masomo Uzamili ( ) Digrii ( )
3. Aina ya shule Kutwa ( ) Bweni ( )

**SEHEMU YA B.**

Sehemu hii inadhamiria kukusanya habari kuhusu swala linalotafitiwa.Tia alama (√) pafaapo.

1. Je, utatumia mbinu ya majadiliano katika vikundi darasani? Ndio( ) La ( )
2. Ni shughuli gani zinahusishwa katika kufundishia stadi ya kuzungumza vikundini ?
   Ukariri ( ) Uimbaji ( ) Kuzungumza ( ) Kusoma ( ) Majadiliano ( )
3. Wajibu wako ni upi katika majadiliano katika vikundi?
   Kuongoza ( ) Kuelekeza ( )
4. Kwa maoni yako majadiliano katika vikundi yana manufaa gani?
   Ushirikiano ( ) Kufikirisha ( ) Kuchangiana ( ) Kuelekezana ( )Kuelewana ( )
5. Ni changamoto zipi zinakumba majadiliano katika vikundi?
   Uzembe () Kuchelewa ( )Kutegemeana ( ) Kuzozana ( ) Kutofanya utafiti ( )

**SHUKRANI KWA USHIRIKIANO WAKO**

## KIAMBATISHO III: MTIHANI KWA WANAFUNZI TEULIWA

Maswali katika mtihani huu yatalenga kutathmini stadi ya kuzungumza. Maswali haya yalijibiwa na kundi husishwa na kundi lisilohusishwa. Yanalenga kuelewa kiwango cha umilisi wa stadi hii miongoni mwa wanafunzi kabla na baada ya kutumia majadiliano vikundini. Mtihani huu pia ulifanywa na makundi yote kama mtihani wa pilli. Mtihani huu ni wa wanafunzi wa kidato cha pili katika shule teuliwa. Kipindi kati ya mtihani wa kwanza na wa pili ni miezi miwili; wa kwanza ukifanywa mwanzoni mwa muhula na wa pili baada ya wanafunzi wateuliwa kuhusishwa katika majadiliano ya vikundi. Alama zote katika mtihani ni hamsini.

1. (i) Tamka vitate vifuatavyo; (a) Futa/vuta (b) suka/shuka (Alama 4)
   (ii) Tamka kitanza ndimi hiki; Wanawali wale wa Liwali hawali wali wa Liwali wao ( Alama 6)
2. Taja maneno yenye maana sawa na; (i) barabara (ii) mvulana (Alama 4)
3. Tegea wanafunzi wengine kitendawili wakishindwa kutegua wakupe mji kisha uwape jibu. ( Alama 4 )
4. Tunga sentensi inayoonyesha; (i) Swali (ii) Mshangao (Alama 6)
5. Simulia wanafunzi wengine kisa kifupi ulichoshuhudia. ( Alama 10)
6. Igiza mazungumzo ya mhubiri. ( Alama 10 )
7. Tolea wanafunzi wengine malumbano ya utani. ( Alama 6 ).

**KIAMBATISHO IV: ALAMA WASTANI ZA MTIHANI WA KWANZA KATIKA SHULE SITA TEULIWA.**

| SHULE | KUNDI | IDADI | ALAMA WASTANI X/50 | ASILIMIA% |
|---|---|---|---|---|
| A | Husishwa | 22 | 30 | 60 |
| | Lisilohusishwa | 21 | 32 | 64 |
| B | Husishwa | 15 | 28 | 56 |
| | Lisilohusishwa | 16 | 30 | 60 |
| C | Husishwa | 21 | 35 | 70 |
| | Lisilohusishwa | 20 | 33 | 66 |
| D | Husishwa | 15 | 34 | 68 |
| | Lisilohusishwa | 14 | 29 | 58 |
| E | Hsishwa | 19 | 28 | 56 |
| | Lisilohusishwa | 18 | 31 | 62 |
| F | Husishwa | 23 | 33 | 66 |
| | Lisilohusishwa | 24 | 32 | 64 |

**KIAMBATISHO V: ALAMA WASTANI ZA MTIHANI WA MWISHO KATIKA SHULE SITA TEULIWA.**

| SHULE | KUNDI | IDADI | ALAMA WASTANI X/50 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|
| A | Husishwa | 22 | 41 | 82 |
| | Lisilohusishwa | 21 | 33 | 66 |
| B | Husishwa | 15 | 35 | 70 |
| | Lisilohusishwa | 16 | 31 | 62 |
| C | Hsishwa | 21 | 42 | 84 |
| | Lisilohusishwa | 20 | 33 | 66 |
| D | Husishwa | 15 | 40 | 80 |
| | Lisilohusishwa | 14 | 30 | 60 |
| E | Husishwa | 19 | 36 | 72 |
| | Lisilohusishwa | 18 | 30 | 60 |
| F | Husishwa | 23 | 38 | 76 |
| | Lisilohusishwa | 24 | 32 | 64 |

# KIAMBATISHO VI: BARUA YA KIBALI KUTOKA CHUONI

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 020 - 8704150

Our Ref: E55/CE/23556/11

Date: 18th June, 2015

The Principal Secretary,
Higher Education, Science & Technology,
P.O. Box 30040,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION MAGARE DANIEL YUVINALIS– REG. NO. E55/CE/23556/11

I write to introduce Mr. Magare Daniel Yuvinalis who is a Postgraduate Student of this University. He is registered for M.Ed degree programme in the **Department of Educational Communication and Technology.**

Mr. Magare intends to conduct research for a M.Ed proposal entitled, **"Matumizi ya Majadiliano Katika Vikundi Kufundisha Stadi ya Kuzungumza Katika Shule za Upili Tarafa ya Mosocho Kaunti ya Kisii, Kenya."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

MRS. LUCY N. MBAABU
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

AM/ewm

## KIAMBATISHO VII: BARUA YA UTAMBULISHO

Magare Daniel Yuvinalis,
Chuo Kikuu cha Kenyatta,
S.L.P. 43844-00100.
Kenya.
2, Septemba 2015.

Kwa yeyote anayehusika,
Bwa/Bi,

**KUH: KIBALI CHA KUKUSANYA DATA KATIKA SHULE YAKO**

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Elimu, Idara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Elimu. Kama moja wapo ya mahitaji ya digrii yangu ya uzamili, ninahitajikla kufanya utafiti nyanjani kuhusu mbinu ya majadiliano katika vikundi miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili, Tarafa ya Mosocho, Kaunti ya Kisii, Kenya.

Nina furaha kukufahamisha kuwa shule yako ni miongoni mwa shule zilizoteuliwa kujumuishwa katika utafiti wangu. Nakusihi uwezeshe ukusanyaji wa data kwa kujazwa hojaii iliyoambatanishwa na barua hii. Nitafurahi sana ikiwa utajaza hojaji hii kwanzia Oktoba hadi Novemba 2015 na kuirudisha kabla ya mwisho wa muhula.

Kwa niaba yangu, wasimamizi wangu, Chuo Kikuu cha Kenyatta, ninaahidi kuwa data, itakayokusanywa itatumiwa kwa minajili ya utafiti na haitatolewa kwa mtu mwingine usiwe na hofu kuijaza. Nakala ya mwisho ya utafiti huu unaweza kuipata utakapoihitaji.

Asante Sana kwa ushirikiano wako katika mchakato huu wa utafiti.

Ndimi wako mwaminifu,

Magare Daniel Yuvinalis


E55/CE/23556/2011

Rununu: 0713330179


Nakala Kwa:

1. Mkuu wa Elimu Kaunti ya Kisii
2. Mkurugenzi wa Elimu Kaunti ya Kisii

## KIAMBATISHO VIII: RAMANI YA KISII YA KATI



# KIAMBATISHO IX: SHULE ZA SEKONDARI KISII YA KATI



# KIAMBATISHO X: LESENI YA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. DANIEL YUVANALIS MAGARE***
**of KENYATTA UNIVERSITY, 0-30200**
**Kitale,has been permitted to conduct**
**research in *Kisii County***

**on the topic: *MATUMIZI YA MAJADILIANO KATIKA VIKUNDI KUFUNDISHIA STADI YA KUZUNGUMZA KATIKA SHULE ZA UPILI***

**for the period ending:**
***30th September,2016***

**Permit No : NACOSTI/P/15/1820/7894**
**Date Of Issue : 2nd October,2015**
**Fee Recieved :Ksh 1,000**



.......................................
***Applicant's Signature***

.......................................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

## KIAMBATISHO XI: KIBALI KUTOKA NACOSTI

NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone: +254-20-2213471,
2241349, 310571, 2219420
Fax: +254-20-318245, 318249
Email: secretary@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No.

Date:
2nd October, 2015

**NACOSTI/P/15/1820/7894**

Daniel Yuvanalis Magare
Kenyatta University
P.O. Box 43844-00100
**NAIROBI.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Matumizi ya majadiliano katika vikundi kufundishia stadi ya kuzungumza katika shule za upili,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kisii County** for a period ending **30th September, 2016.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Kisii County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are expected to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**DR. S. K. LANGAT, OGW**
**FOR: DIRECTOR GENERAL/CEO**

Copy to:

COUNTY COMMISSIONER
KISII COUNTY
Authorized
29/12/2015

The County Commissioner
Kisii County.

The County Director of Education
Kisii County.

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KISII
P O Box ... KISII
Date 28/12/2015